

**MIKAKATI YA UTOUPOLE KATIKA TAMTHILIA YA *PANGO* YA KYALLO
WADI WAMITILA**

NA

**MICHAEL WAFULA
NAMBARI YA USAJILI
C50/85049/2016**

WASIMAMIZI:

PROF. JOHN HABWE

NA

PROF. IRIBE MWANGI

**TASNIFU HII IMETOLEWA KWA MADHUMUNI YA KUTOSHELEZA BAADHI YA
MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA MASOMO YA KISWAHILI IDARA
YA KISWAHILI, CHUO KIKUU CHA NAIROBI.**

NOVEMBA, 2019

UNGAMO

Nakiri kuwa tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijawahi kutolewa katika chuo kingine chochote, kwa minajili ya kutosheleza mahitaji ya shahada ya uzamili

Sahihi.....

Tarehe.....

MICHAEL WAFULA

Mtahiniwa (C50/85049/2016)

Tasnifu hii imetolewa ili kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa na Chuo Kikuu cha Nairobi.

Sahihi.....

Tarehe.....

PROF. JOHN HABWE

(Mtahini)

Sahihi.....

Tarehe.....

PROF. IRIBE MWANGI

(Mtahini)

TABARUKU

Kwako wewe mama yangu mpendwa: Mary Shimuli. Ulinilea, ukajinyima ili kunisomesha, ukaniekeleza na kunipa mizungu ya kukabili miamba ya maisha.

Kwako mke wangu: Teresiah Wanjira Wachira pamoja na wanetu Favour Imani Wafula na Samuel Baraka Wafula mlioniamini na kunitunuku rasilimali za familia ili niyaendeleze masomo haya ya uzamili, pamoja na mapenzi yenu kwangu, maombi na uvumilivu unimenipa nguvu za kuendelea na kazi hii.

SHUKRANI

Kwanza, kabisa, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa fadhili zake na kunipatia nguvu za kukabiliana na changamoto mbalimbali wakati wa kuitafitia mada hii. Sina budi kukiri bayana kuwa, Mwenyezi Mungu amenipatia kariha na hamu ya kuendelea kuisukuma kazi hii hasa pale nilihisi kulemewe na changamoto za maisha. Kwa msingi huu, natangaza kuwa, shukrani, utukufu na heshima ni zake.

Pili, ntoa shukrani zangu za dhati kwa wasimamizi wangu; Prof. John Habwe na Prof. Iribe Mwangi kwa kunishika mkono na kunielekeza katika kuiandaa kazi hii kuanzia mwanzo hadi mwisho. Kwa hakika, mmenielekeza na kunifunza mengi kuhusu utafiti ambayo isingekuwa nyinyi ingekuwa vigumu kuyaelewa. Asanteni kwa uvumilivu ambao mmekuwa nao kwangu katika kunikosa na kunielekeza hadi nikafikia kiwango hiki. Shukrani sana na Mungu awabariki.

Vilevile, shukrani tumbi nzima ziwaendee wahadhiri wote katika Chuo Kikuu cha Nairobi, Idara ya Kiswahili. Mafunzo, maelekezo na ushauri wenu ulinitia motisha na ilhamu ya kuifanya kazi hii na kuikamilisha. Wahadhiri hawa ni pamoja na, Prof. Habwe, Prof. Iribe, Prof. Kithaka, Prof. Wamitila, Dkt. Zaja, Prof. Abdulaziz, Prof. Kineene wa Mutiso, Prof. Mbuthia, Prof. Rayya Timamy, Prof. Mwenda Mbatiah, Dkt. Mukhwana, Dkt. Swaleh, Dkt. Mungania, Dkt. Jerono, Dkt. Jefwa Mweri, Mwl. Sanja, Bw. Ongarora na Bi. Mary Ndung'u. Nimejifunza mengi sana kutokana na uelekezi wenu tangu enzi nikisomea shahada ya kwanza chuoni humu almaarufu “shahada ya ukapera.” Nawashukuru nyote na Mungu awabariki kwa kazi nzuri mnayoifanya.

Ningependa kumshukuru mke wangu Terry sio tu katika kutoa mchango wake wa hali na mali, bali pia kwa kuvumilia upweke siku zote nilipokuwa nimezama maktabani kuishughulikia kazi hii. Nawashukuru pia watoto wetu Favour Imani Wafula na Samuel Baraka Wafula kwa kunipa ilhamu ya kusoma zaidi ili niwe kielelezo chema kwao. Nawashukuru ndugu na jamaa wote kwa kunipa moyo kila mara hasa mlipokuwa mkiniambia, “ Bwana, jikaze umalize mradi huu.” Pia nawashukuru wasomi wote tuliowahi kusoma pamoja kuanzia shule ya msingi hadi chuo kikuu. Kwa sababu mlikuwa chachu katika hamu yangu ya kuzamia taaluma ya Kiswahili. Mungu aonaye kwa siri awaneemeshe. Mwisho, nawashukuru wanafunzi wote niliowahi kutangamana nao darasani nikiwafunza kuanzia Shule ya msingi ya High Peak, Shule ya upili ya North Gate na Njonjo, kwani daima walikuwa chachu yangu ya kuwa bora zaidi katika taaluma ya Kiswahili.

IKISIRI

Utafiti huu unalenga kubainisha namna mtazamo wa kipragmatiki unaweza kutumiwa kuihakiki kazi ya fasihi. Ili kufanikisha lengo hili, tamthilia ya Pango iliteuliwa kimakusudi ili ilitupatie data ya utafiti huu. Data ya utafiti huu ilitokana na uchunguzi wa kauli za wahusika mbalimbali katika tamthilia teule na kuzichanganua kwa msingi wa Nadharia ya Utoupole ya Culpeper (1996). Lengo la kwanza la utafiti huu lilikuwa kubainisha mikakati ya utoupole ambayo inatumiwa na wahusika wanapoingiliana na wenzao ili kufanikisha mazungumzo yao. Matokeo ya utafiti huu yanaonyesha kuwa wahusika katika tamthilia ya Pango wanatumia mikakati ya utoupole ili kudhuru nyuso za wenzao ili kudhoofisha au kuvunja mawasiliano miongoni mwao. Lengo la pili la utafiti huu lilikuwa kubainisha namna mikakati ya utoupole inayotumiwa na wahusika katika tamthilia ya *Pango* inachangia katika ukuzaji wa sifa zao. Matokeo ya utafiti huu yanaonyesha kuwa sifa za wahusika mbalimbali zikiwa ni pamoja na hasi na chanya zimebainika kupitia matumizi yao ya mikakati ya utoupole. Vilevile, utafiti huu ulilenga kubainisha namna mikakati ya utoupole inayotumiwa na wahusika inaendeleza maudhui katika tamthilia ya *Pango*. Matokeo ya utafiti huu yanaonyesha kuwa mikakati ya utoupole inayotumiwa na wahusika mbalimbali inaendeleza maudhui mbalimbali.

MAELEZO YA DHANA

Upole –Tutatumia dhana hii katika utafiti huu kurejelea matumizi ya lugha katika mazungumzo ambayo yanazingatia heshima na hali ya kujali msikilizaji.

Utoupole – Katika utafiti huu, tutatumia dhana hii kurejelea matumizi ya lugha ambayo yanadhihirisha utovu wa adabu na heshima, kwa msikilizaji kwa lengo la kuhasiri uso wa wahusika katika mazungumzo na kusababisha kudhoofika kwa mawasiliano au hata kuvunjika kwa mawasiliano.

Vitendo vinavyotishia uso – matamshi yanayoweza kumkasirisha mzungumzaji au msikilizaji wakati wa mazungumzo na kusababisha kuvunjika kwa mawasiliano.

ORODHA YA VIFUPISHO AMBAVYO VIMETUMIKA

Uk. – ukurasa

TUKI – Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili

YALIYOMO

UNGAMO	ii
TABARUKU	iii
SHUKRANI	iv
IKISIRI	v
MAELEZO YA DHANA	vi
ORODHA YA VIFUPISHO AMBAVYO VIMETUMIKA	vii
SURA YA KWANZA	1
1.1 UTANGULIZI.....	1
1.2 TATIZO LA UTAFIGI.....	3
1.3 MASWALI YA UTAFIGI.....	3
1.4 MADHUMUNI YA UTAFIGI.....	3
1.5 SABABU ZA KUCHAGUA MADA.....	4
1.6 UPEO NA MIPAKA.....	4
1.7 UMUHIMU WA UTAFIGI.....	4
1.8 UDURUSU WA YALIYOANDIKWA KUHUSU SOMO.....	5
1.8.1 Yaliyoandikwa kuhusu nadharia ya utafiti.....	5
1.8.2 Yaliyoandikwa kuhusu mada ya utafiti.....	8
1.9 MISINGI YA KINADHARIA.....	10
1.9.1 DHANA YA USO.....	10
1.9.2 USO CHANYA NA USO HASI.....	10
1.9.3 NADHARIA YA UPOLE.....	11
1.9.4 NADHARIA YA UTOUPOLE.....	13
1.9.4.1 Mkakati hasi wa utoupole.....	13
1.9.4.2 Mkakati chanya wa utoupole.....	14
1.9.4.3 Mkakati ndani ya rekodi wa utoupole.....	14
1.9.4.4 Matumizi ya kejeli au Mkakati nje ya rekodi.....	15
1.9.4.5 Kutowasilisha chochote.....	15
1.0.1 MBINU ZA UTAFIGI.....	16
1.0.2 Uteuzi wa sampuli.....	16
1.0.3 Mbinu za kukusanya data.....	17
1.0.4 Uchanganuzi wa data.....	17

1.0.5 Uwasilishaji wa matokeo ya data.....	17
SURA YA PILI.....	18
MATUMIZI YA MIKAKATI YA UTOUPOLE KATIKA TAMTHILIA YA <i>PANGO</i>	18
2.1 UTANGULIZI	18
2.2 Sinopsia ya tamthilia ya <i>Pango</i>	18
2.3 Matumizi ya Mkakati Hasi wa Utoupole	21
2.3.1 Mzungumzaji Kumrejelea Msikilizaji kwa Njia Hasi.....	21
2.3.2 Mzungumzaji kuingilia faragha ya msikilizaji.....	23
2.3.3 Mzungumzaji Kumkebehi Msikilizaji Wake	24
2.3.4 Mzungumzaji Kuntisha Msikilizaji Wake	25
2.4 Matumizi ya Mkakati Chanya wa Utoupole	26
2.4.1 Mzungumzaji Kutotaka Kujihusisha na Msikilizaji Wake	26
2.4.2 Mzungumzaji Kumtusi Msikilizaji Wake	27
2.4.3 Mzungumzaji Kutumia Maneno ya Miiko Katika Mazungumzo	28
2.4.4 Mzungumzaji Kutomwonea Msikilizaji Huruma.....	29
2.4.5 Mzungumzaji Kutafuta Kutokubaliana na Msikilizaji Wake.....	30
2.4.6 Mzungumzaji kumpa msikilizaji wake utambulisho usiofaa	31
2.4.7 Mzungumzaji kumpuuza msikilizaji wake.....	33
2.5 Mkakati ndani ya rekodi wa utoupole.....	33
2.6 Matumizi ya kejeli au Mkakati nje ya rekodi.....	36
2.7 Kutowasilisha chochote	37
2.7.1 Kitendo cha kutoshukuru	38
2.7.2 Kuondoka bila ya kuaga.....	38
2.7.3 Kitendo cha kutojibu salamu.....	39
2.8 HITIMISHO.....	40
SURA YA TATU.....	41
3.1 UTANGULIZI	41
3.2 Mchango wa mikakati ya utoupole hasi katika ukuzaji wa wahusika.....	41
3.3 Mchango wa mikakati chanya ya utoupole katika ukuzaji wa wahusika.....	45
3.4 Mchango wa mkakati ndani ya rekodi wa utoupole katika kuzikuza sifa za wahusika	48
3.5 Mchango wa matumizi ya kejeli katika kuzikuza sifa za wahusika.....	50
3.6 Mchango wa kutowasilisha chochote katika kuzikuza sifa za wahusika	51

3.7 Hitimisho.....	52
SURA YA NNE	53
MIKAKATI YA UTOUPOLE NA UKUZAJI WA MAUDHUI	53
4.1 UTANGULIZI.....	53
4.2 Mchango wa mkakati hasi wa utoupole katika kukuza maudhui.....	53
4.3 Mchango wa mkakati chanya wa utoupole katika kukuza maudhui.....	55
4.4 Mchango wa mkakati ndani ya rekodi wa utoupole katika ukuzaji wa maudhui	58
4.5 Mchango wa matumizi ya kejeli katika kukuza maudhui.....	60
4.6 Mchango wa mkakati wa Kutowasilisha chochote katika kukuza maudhui.....	61
4.7 Hitimisho.....	62
SURA YA TANO	63
HITIMISHO NA MAPENDEKEZO	63
5.1 Utangulizi.....	63
5.2 Kutathmini Ufanisi wa Madhumuni ya Utafiti	63
5.3 Changamoto za Utafiti	67
5.4 Mapendekezo	67
MAREJELEO	68

SURA YA KWANZA

1.1 UTANGULIZI

Mawasiliano ni mchakato changamano ambao hujumuisha vipengele mbalimbali ili kuukamilisha. Kwanza kuna mtumaji ambaye ni mwenye ujumbe ambao anataka kuupitisha. Naye mpokezi ni mtu ambaye anapokea ujumbe kutoka kwa mtumaji. Kwa kuwa binadamu hawana uwezo wa kuingia kwenye ubongo wa wengine na kupata ujumbe huo, inambidi mtumaji kuteua njia ambayo itamwezesha kupitisha ujumbe wake hadi kwa mpokezi. Lugha ya binadamu ndio huwa njia kuu ya kupitisha ujumbe huo.

Buliba, A. na wengine (2006) wanasema kuwa lugha ni chombo cha mawasiliano. Hii ina maana kuwa binadamu huhitaji lugha ili kuweza kuwasiliana na wengine katika jamii anamoishi. Hata hivyo lugha ambayo mtumaji anatumia katika mawasiliano huweza kuathiri ujumbe utakavyopokelewa na mpokezi wake. Lugha ambayo inatumiwa inaweza kumsaidia mtumaji kuhifadhi uso wake na wa wasikilizaji wake au kudhuru uso wa wahusika katika mawasiliano.

Kulingana na Brown na Levinson (1987) mtu anapotumia lugha ambayo humsaidia kuokoa uso wake na wa wengine katika mawasiliano huwa anazingatia suala la upole. Naye Culpeper (1996) anasema kuwa upo wakati mwingine ambapo mtumaji hutumia lugha inayodhuru au kuhasiri uso. Hali hii inapodhihiri mtumaji huwa anazingatia suala la utoupole. Vitendo vinavyotishia uso ni pamoja na mtu kumhusisha mwenzake na utambulisho hasi, kutisha, kuonya, kuamuru na hata kuingilia faragha ya mwingine. Hali hizi humnyima mtu uhuru wa kutenda anavyotaka binadamu.

Upole husaidia kuanzisha na kudumisha mawasiliano miongoni mwa wahusika ilhali suala la utoupole hutumiwa ili kusababisha migongano ya kijamii ambayo husababisha kuvunjika kwa mawasiliano. Kwa hivyo ikiwa mawasiliano hayamvutii mlengwa anaweza kutumia mikakati ya utoupole ili kuyakatisha. Hata hivyo ili kitendo kifasiriwa kama chenye upole au chenye utoupole hutegemea lengo la msikilizaji na muktadha. Upole au utoupole huweza kujitokeza kupitia lugha inayotumika katika mawasiliano au ishara za mwili kwa mfano umbali baina ya wahusika au hata kunyanyua nyusi.

Utafiti huu utajikita tu katika kauli za wahusika bila kuhusisha matendo ya wahusika. Katika utafiti huu tutaongozwa na mikakati ya utoupole kama ambavyo ilipendekezwa na Culpeper (1996). Mikakati hii ni pamoja na : mikakati chanya ya utoupole, mikakati hasi ya utoupole, mikakati ndani ya rekodi ya utoupole, matumizi ya kejeli na kutowasilisha chochote. Kwa ujumla, nadharia ya Culpeper ya utoupole inatambua mikakati mitano ya utoupole ambayo wazungumzaji huweza kuitumia ili kudhuru uso wa wenzao katika mazungumzo. Kwa upande mwingine nadharia ya upole ya Brown na Levinson (1987) inatambua mikakati minne ya upole ambayo huweza kutumiwa na wazungumzaji katika mawasiliano ili kuokoa nyuso zao na za wengine. Mikakati hii ni pamoja na: mkakati chanya wa upole, mkakati hasi wa upole, mkakati ndani ya rekodi wa upole na mkakati nje ya rekodi wa upole.

Nchini Kenya, utanzu wa tamthilia hauna historia ndefu si kama riwaya na ushairi. Utanzu wa tamthilia ulianza kujitokeza baina ya mwaka wa 1950 na 1957. Wakati huo tamthilia ambazo ziliandikwa ni pamoja na *Mgeni Karibu* (1957), *Afadhali Mchawi* (1957) zake Graham Hyslop na *Nakupenda Lakini* (1957) ya Henry Kuria ambaye alikuwa mwanafunzi wa Graham Hyslop. Katika tamthilia za wakati huu maudhui hayakuwa ya kukweza mila na tamaduni za kiafrika ila yalitukuza ukoloni. Maudhui haya yalilenga kumrahishia mkoloni utawala wake. Katika kipindi cha ukoloni tamthilia zilizoandikwa zilijikita katika ulimbwende uliokusudia kufurahisha tu. Tamthilia hizi hazikuonyesha uhalisia wowote katika jamii.

Waandishi wa tamthilia ya Kiswahili baada ya uhuru kama Hussein, E. (1971) katika *Wakati Ukuta* walianza kushughulikia maudhui ya hali halisi ya maisha ya wakati huo. Haya maudhui yalijumuisha masuala ya ukombozi wa kisiasa pamoja na kuwajibika kwa viongozi. Katika kipindi hiki tamthilia zilimulika matatizo yaliyoikumba jamii baada ya ukoloni. Katika kipindi hiki tamthilia zilichukua mwelekeo wa nadharia ya usasa na usasaleo.

Wamitila ni miongoni mwa waandishi ambao wameandika katika kipindi cha baada ya uhuru. Tamthilia yake ya kwanza ya *Wingu la Kupita* (1999), imekitwa katika misingi ya fasihi ya kimajaribio. Katika tamthilia yake ya pili ya *Pango* (2003), Wamitila ameangazia hali halisi ya kijamii kisiasa ambapo Katango ambaye ni mwanamke anajitokeza kuwania kuwa mlinzi wa Pango sawa na wanaume. Katika *Sumu ya Bafe* (2006), Wamitila ameisuka tamthilia hii kijazanda ambapo sumu inarejelea athari za ukoloni naye bafe ni mkoloni mwenyewe. Katika tamthilia hii inabainika kuwa, hata kama jamii imejitwalia uhuru bado kuna athari za ukoloni

katika jamii. Kupitia jazanda ya sumu ya bafe tunapata maudhui makuu ya tamthilia hii ya ukoloni mambo leo.

1.2 TATIZO LA UTAFITI

Suala la upole na umuhimu wake katika kuanzisha na kudumisha mahusiano katika jamii limechunguzwa na watafiti wengi. Watafiti hawa hasa wamekuwa wakiongozwa na nadharia ya upole ya Brown na Levinson (1987). Utafiti huu unakusudia kuchunguza ikiwa suala la utoupole limechunguzwa na ikiwa suala hili lina mchango wowote katika uhakiki wa kazi za fasihi. Katika utafiti huu mtafiti atachunguza nafasi ya mikakati ya utoupole katika kufanikisha drama akitumia tamthilia ya *Pango* kama kielelezo.

Utafiti huu unakusudia kuziba pengo katika Kiswahili kwa kuonyesha namna nadharia ya pragmatiki inaweza kutumiwa kuhakiki kazi za fasihi. Ni kutokana na kuwepo kwa pengo la suala la utoupole kutozamiwa kwa kina hasa katika fasihi andishi ndipo utafiti huu unapata misingi yake. Kwa uelewa wangu ni kuwa hakuna utafiti ambao umefanywa kuhusu suala la utoupole katika fasihi andishi ya Kiswahili hasa tamthilia ya Wamitila, K.W. ya *Pango*. Msuko wa tamthilia husukumwa mbele kutokana na mazungumzo au dayalojia miongoni mwa wahusika. Kwa hivyo uchunguzi wa lugha inayotumika katika tamthilia ni muhimu sana, kwani tamthilia zinapoandikwa hokusudiwa kuigizwa jukwaani. Zinapoigizwa huwa sanaa tendi na kwa hivyo huakisi lugha inavyoitumikia jamii katika shughuli halisi zake za kila siku katika kuanzisha na kudumisha mahusiano yake mbalimbali au hata kuvunja mahusiano mbalimbali.

1.3 MASWALI YA UTAFITI

Katika utafiti huu mtafiti anakusudia kuyapata majibu ya maswali haya:

- a) Je, ni mikakati ipi ya utoupole inayotumiwa na wahusika katika tamthilia ya *Pango*?
- b) Mikakati ya utoupole inachangia vipi kuzikuza sifa za wahusika?
- c) Mikakati ya utoupole ina mchango upi katika kuendeleza maudhui katika tamthilia ya *Pango*?

1.4 MADHUMUNI YA UTAFITI

Katika utafiti huu, ili kuchunguza namna ambavyo wahusika wanatumia mikakati mbalimbali ya utoupole katika tamthilia ya *Pango* mtafiti ataongozwa na madhumuni yafuatayo:

1. Kubainisha mikakati ya utoupole ambayo inatumiwa na wahusika wanapoingiliana na wenzao ili kufanikisha mazungumzo yao.
2. Kuchunguza namna mikakati ya utoupole inayotumiwa na wahusika katika tamthilia ya *Pango* inachangia katika ukuzaji wa sifa zao.
3. Kubainisha namna mikakati ya utoupole inayotumiwa na wahusika inaendeleza maudhui katika tamthilia ya *Pango*.

1.5 SABABU ZA KUCHAGUA MADA

Mtafiti aliteua mada hii kwa sababu itampatia fursa ya kutumia mtazamo wa kipragmatiki kuihakiki kazi ya fasihi. Na nadharia hii ndiyo iliyo na uzito wa kuangalia suala la utoupole: tunaamini kuwa mtazamo huu utapanua uga wa kuangalia masuala ya kifasihi. Tulateua tamthilia kwa sababu katika Afrika Mashiriki filamu hazijakuzwa kama Ulaya. Hivyo basi tamthilia inaingiliana moja kwa moja na maisha ya jamii. Tamthilia ya *Pango* ya Wamitila ilituliwa kwa sababu imetumia mitazamo ya utoupole kwa wingi kwa hivyo inaweza kutumiwa kama kielelezo cha mikakati ya utoupole ya Culpeper.

1.6 UPEO NA MIPAKA

Kimsingi utafiti huu unachunguza jinsi ambavyo wahusika katika tamthilia ya *Pango* (Wamitila, K.W. 2003) wanatumia mikakati ya utoupole wanapoingiliano na wenzao. Utafiti huu unahusisha mikakati ya utoupole wala si mikakati ya upole. Aidha, tulichunguza jinsi ambavyo mikakati hii ya utoupole inakuza sifa za wahusika na kuendeleza maudhui katika tamthilia ya *Pango* tuliyoiteua. Katika uchunguzi huu tumejikita katika isimumatini na tuliongozwa na mihimili ya nadharia ya utoupole kama ilivyoelezwa na Culpeper (1996). Katika utafiti huu tulionyesha jinsi mawazo ya kiisimu yanavyoweza kutumiwa katika kuchambua kazi za fasihi. Katika kutekeleza hili, pengo lililopo baina ya isimu na fasihi litapungua. Swali la kimsingi ambalo tulijiuliza ni je, dhana ya utoupole ina mchango gani katika uchambuzi wa tamthilia?

1.7 UMUHIMU WA UTAFITI

Utafiti huu unachunguza namna mikakati ya utoupole inatumiwa na wahusika katika tamthilia ya *Pango* ya K.W. Wamitila katika maingiliano yao ili kudhuru uso wa wenzao na kusababisha migongano miongoni mwao. Utafiti huu ni muhimu kwa watafiti wa lugha ya Kiswahili kwani

matokeo yake yatawatia motisha wa kuchunguza diskosi na kauli mbalimbali za wahusika katika kazi nyinginezo za fasihi zikiwemo hadithi fupi, riwaya na hata novela.

Pili ni, tamthilia ya *Pango* imefanyiwa tafiti nyingi ila kulingana na uelewa wetu ni kuwa haijawahi kufanyiwa utafiti wa semantiki na pragmatiki. Kwa msingi huu basi utafiti huu utakuwa muhimu katika kuziba pengo la kielimu kati ya fasihi ya Kiswahili na semantiki na pragmatiki. Hii ni kwa kuwa isimu huingiliana na fasihi na hakuna utanzu unaoweza kukaa pekee yake.

Tatu ni, utafiti huu ni muhimu kwa kuwa unaonyesha namna utoupole unavyoweza kutumiwa na wahakiki katika kuchimuza sifa za wahusika na maudhui katika matini za fasihi. Hili linabainisha kuwa zaidi ya kutumia nadharia za fasihi kama vile: ufeministi, umaksi, sosholojia, uhalisia na nyinginezo pia nadharia za semantiki na pragmatiki zinaweza kutumiwa katika kuchanganua kazi za fasihi.

Nne ni, tamthilia husukumwa mbele na dayalojia baina ya wahusika. Kwa hivyo kuchunguza lugha inyotumiwa na wahusika ni muhimu. Mwisho ni kuwa utafiti huu pia ni muhimu kwani unaichangizia nadharia ya utoupole kimaarifa. Hali hii itaipanua zaidi kimawanda hasa ikizingatiwa kwamba suala la utoupole halijachunguzwa kwa kina sana.

1.8 UDURUSU WA YALIYOANDIKWA KUHUSU SOMO

Katika sehemu hii tutagawanya yaliyoandikwa kuhusu somo katika sehemu mbili: Kwanza yaliyoandikwa kuhusu nadharia ya utafiti na yaliyoandikwa kuhusu mada ya utafiti.

1.8.1 Yaliyoandikwa kuhusu nadharia ya utafiti

Katika sehemu hii tutaangazia mawazo ya wataalamu mbalimbali kuhusu nadharia ya utoupole. Nadharia ya utoupole ya Culpeper (1996) imechangiziwa kimawazo na wataalamu mbalimbali. Kuna watafiti ambao wameiwekea nadharia hii misingi kama vile Brown na Levinson (1987) huku wengine kama vile Bousfield (2008) wameihakiki nadharia hii. Pia Culpeper mwenyewe katika kazi za baadaye ameiendeleza nadharia hii. Brown na Levinson (1987) ndio walioasisi nadharia ya upole. Katika kufafanua nadharia hii walisema kuwa kuna matendo ambayo hutishia uso wa msemaji na msikilizaji ambayo ni pamoja na: kuonya, kutisha, kuamuru, kudunisha au kuzungumzia mada ambazo ni mwiko katika jamii husika miongoni mwa mengine. Matendo haya hudhuru uso wa msemaji na msikilizaji na kusababisha migongano ya kijamii na kuvunjika

kwa mawasiliano. Pia katika kueleza mikakati yao ya upole hasa upole hasi, waliiwekea nadharia ya utoupole misingi. Kulingana na Culpeper (1996) utoupole hujumuisha matendo yote yanayotendwa kimakusudi na msemaji kwa msikilizaji akiwa na lengo la kudhuru uso na kusababisha kuvunjika kwa mawasiliano. Nadharia ya utoupole ina mizizi yake katika nadharia ya upole.

Lachenict (1980) anatambua mikakati minne ya utoupole ambayo hunuia kumkasirisha msikilizaji katika mazungumzo. Mikakati anayoipambanua ni pamoja na mkakati nje ya rekodi wa utopole, mkakati ndani ya rekodi wa utoupole, mkakati hasi wa utoupole na mkakati chanya wa utoupole. Kulingana na Lachenict mkakati nje ya rekodi wa utoupole hujumuisha matumizi ya lugha ya matusi na pia kejeli katika mazungumzo. Nao mkakati ndani ya rekodi wa utoupole hujumuisha matendo yanayotishia uso na kukatisha mazungumzo au hata wakati mwingine kuingilia mazungumzo ya wengine. Mkakati chanya wa utoupole hujumuisha msemaji kutomtambua msikilizaji kama sehemu ya kundi katika jamii. Na mwisho katika mkakati hasi wa utoupole huhusisha mzungumzaji kumshurutisha msikilizaji wake kutenda jambo fulani au msemaji kuingilia faragha ya msikilizaji wake na kudhuru hadhi yake katika jamii. Mawazo haya ya Lachenict (1980) yanaelekea kulandana na mawazo ya Culpeper (1996) isipokuwa kwamba Culpeper amefafanua suala la utoupole kwa kina kuliko Lachenict. Hata hivyo mawazo ya Lachenict yana umuhimu katika utafiti huu kwa sababu yanaingiliana na mawazo ya Culpeper.

Eelen (2001) anasema kuwa utoupole katika mazungumzo ni suala ambalo ni vigumu kuliepuka. Anaeleza kwa kutolea mfano hali ambayo inaweza kusababisha utoupole katika mawasiliano. Anasema kwamba utoupole unaweza kutokea katika hali ambapo mtu anakosa kujibu salamu na badala yake anahiari kuwa kimya. Vile vile Culpeper (2005) alitoa mfano unaoana na wa Eelen aliposema kuwa utoupole waweza kutokea katika hali ambapo mtu anapokea zawadi kisha anakosa kushukuru. Mawazo ya Eelen na Culpeper ni muhimu katika utafiti huu kwani yanatuongoza katika kutambua mikakati ya utoupole hasa katika mkakati wa kutowasilisha chochote.

Kwa kuwa suala la utoupole haliwezi kuepukika katika mawasiliano, Bousfield na Locher (2008) wanashikilia kuwa msikilizaji anapokabiliwa na vitendo vinavyodhuru uso anaweza: kukubali vitendo hivyo, kukabiliana navyo au hata anaweza akaamua kuwa kimya. Mawazo yao yaungwa mkono na Culpeper (2003) anayependekeza kuwa msikilizaji anapokabiliwa na hali ya utoupole

katika mawasiliano kuna mbinu ambazo anaweza akazitumia ili kukabili hali hii. Mbinu hizi ni kama vile: kukabili vitendo vinavyodhuru uso, kutokabili vitendo vinavyohasiri uso na kuwa kimya. Katika mbinu ya kukabili vitendo vinavyohasiri uso, msikilizaji anaweza kuvikabili kwa namna ya kumshambulia msemaji. Kwa upande wake mbinu ya kutokabili vitendo vinavyohasiri uso kwa kuwa kimya msikilizaji huwa anakubaliana na kauli za msemaji zinazodhihirisha utoupole katika mawasiliano.

Bousfield (2008) anamwunga Culpeper (2003) mkono kwa kusema kuwa msikilizaji hukubali kitendo kinachodhuru uso kutoka kwa mzungumzaji anapokubaliana na kauli za msemaji zinazodhihirisha utoupole katika mazungumzo. Msikilizaji anaweza hata akaomba radhi katika hali ambazo hata hajafanya kosa lolote anapokabiliwa na hali hii.

Kwa ujumla hali za utoupole katika mawasiliano zinaweza kukabiliwa kwa njia zifuatazo: kukubali vitendo vinavyodhuru uso, kukabili vitendo vinavyodhuru uso na kuwa kimya. Kulingana na Bousfield (2008) katika mbinu ya kukubali vitendo vinavyodhuru uso kutoka kwa msemaji, msikilizaji hukubaliana na kauli za mzungumzaji ambazo zinadhihirisha utoupole katika mazungumzo. Hii ina maana kwamba msikilizaji anaweza kuomba msamaha hata katika hali ambazo hajafanya kosa lolote. Katika mbinu ya kukabili vitendo vinavyodhuru uso, msikilizaji hujaribu kutenda vitendo vinavyodhuru uso wa mzungumzaji au hufanya juu chini kujikinga dhidi ya vitendo vinavyohasiri uso wake kutoka kwa mzungumzaji. Katika hali hii ya kukabili vitendo vinavyodhuru uso, msikilizaji anaweza akatumia njia mojawapo kati ya hizi kama zilivyopendekezwa na Culpeper (1996) na Bousfield (2008): Kukabili vitendo vinavyohasiri uso kwa namna ya kujikinga, kukabili vitendo vinavyodhuru uso kwa namna ya kumshambulia mzungumzaji na kuwa kimya.

Katika hali ya kujikinga dhidi ya vitendo vinavyodhuru uso kwa kukabili vitendo vinavyohasiri uso kwa namna ya kujikinga, msikilizaji hukubali vitendo vinavyodhuru uso pengine kwa kujibu maswali yaliyoulizwa na msemaji, kumwambia mzungumzaji mambo yanayonua kuleta hali ya uelewano kati ya msemaji na msikilizaji au hata msikilizaji kumtania mzungumzaji wake. Na katika hali ya kujikinga dhidi ya vitendo vinavyodhuru uso kwa namna ya kumshambulia mzungumzaji, mzungumzaji anapotenda kitendo kinachodhuru uso wa msikilizaji, msikilizaji pia hujibu kwa kutenda kitendo kinachohasiri uso wa mzungumzaji. Kwa hivyo hali hii inapotukia ugomvi mkali husababishwa kati ya mzungumzaji na msikilizaji wake kama vile, mzungumzaji

kumtusi msikilizaji wake naye msikilizaji kukabili hali hii kwa kumtusi mzungumzaji wake. Mawazo ya wataalamu hawa ni muhimu katika utafiti huu kwa sababu yanagusia masuala mbalimbali yanayodhuru uso ambayo ndiyo yanayoshughulikiwa katika utafiti huu.

Nadharia ya utoupole imeendelezwa zaidi na Bousfield na Locher (2008) walipojadili suala la utoupole na mamlaka. Wanasema kwamba wakati mwingine katika uhusiano wa mzungumzaji na msikilizaji huwa wametenganishwa na mamlaka. Mzungumzaji anapokuwa na mamlaka zaidi ya msikilizaji kauli zake huweza kuwa zenye utoupole katika mawasiliano. Mawazo yao yanahusiana na utafiti huu kwa sababu wanazungumzia utoupole na mamlaka na pia utafiti huu unahusu utoupole.

1.8.2 Yaliyoandikwa kuhusu mada ya utafiti.

Katika sehemu hii mtafiti ameshughulikia yaliyoandikwa kuhusu mada ya utafiti. Kuna wale ambao wamefanya tafiti zao wakitumia nadharia ya utoupole iliyoasisiwa na Culpeper (1996) kama vile:

Nyangi (2017), alitafitia suala la utoupole katika filamu za Kiswahili. Kulingana na utafiti wake ni kwamba waigizaji katika filamu nne za Kiswahili alizoziteua walitumia mikakati ndani ya rekodi kwa wingi kuliko mikakati mingine ya utoupole. Utafiti wake una umuhimu katika utafiti huu kwa kuwa unauchangizia kinadharia kwani utafiti wa Nyangi ulitumia nadharia ya utoupole kama huu. Kwa hivyo utatusaidia kuchanganua data kwa kutumia nadharia ya utoupole. Hata hivyo utafiti wa Chacha unatofautiana na utafiti huu kwa kuwa yeye alichunguza suala la utoupole katika filamu za Kiswahili, nao huu unachunguza mikakati ya utoupole katika tamthilia ambao ni utanzu wa fasihi andishi.

Naye Nabella (2015) alichunguza mikakati ya utoupole iliyotumiwa na wahusika wasaidizi kwa wahusika wakuu katika sinema ya *Paranorman*. Utafiti wake una umuhimu kwa utafiti huu kwani unauchangizia mawazo kinadharia. Pia utatusaidia kuchanganua data ambazo tutakusanya. Utafiti wa Nabella ni tofauti na utafiti huu kwa kuwa yeye alijikita katika sinema ya Kiulaya ya *Paranorman* nao utafiti huu unajikita katika tamthilia ya *Pango* ambayo ni fasihi andishi.

Goro (2014) alichunguza namna lugha iliyotumiwa baina ya makondakta na abiria iliibua utoupole uliosababisha kuvunjika kwa mawasiliano baina yao. Goro alifanyia utafiti wake katika

matatu zilizotoka katika jiji la Nairobi kuelekea mtaa wa Dandora. Utafiti wake una uhusiano na utafiti huu kwa sababu tafiti hizi zote mbili zinatumiya nadharia ya utoupole iliyoasisiwa na Culpeper (1996). Utafiti wake utauchangizia mawazo kinadharia utafiti huu na pia kutuelekeza katika kuchanganua data kwa kutumia mikakati ya utoupole.

Kinyua (2015) alichunguza ukiukaji wa kanuni za upole katika riwaya ya *Mhanga Nafsi Yangu*. Utafiti wa Kinyua uliongozwa na nadharia ya upole ya Brown na Levinson (1987) kuchunguza jinsi ambavyo wahusika wanakiuka kanuni za upole katika riwaya hii ili kujenga na kuendeleza maudhui katika riwaya hii. Utafiti huu una umuhimu katika kuuchangizia mawazo utafiti huu kwa sababu vitendo vyote vinavyokiuka kanuni za upole hufasiriwa kama vyenye kudhuru uso wa msikilizaji au msemaji katika mtagusano wa kimazungumzo. Utafiti huu unalenga kuchunguza vitendo hivi vinavyhasiri uso wa mzungumzaji au msikilizaji. Kwa hivyo utafiti huu unapewa uhalali na utafiti wa Kinyua.

Vile vile kuna yaliyoandikwa kimaudhui kuhusu mada ya utafiti. Nyangweso (2017) alichunguza suala la nafasi na athari ya kiongozi wa kike katika tamthilia teule za kiswahili. Katika utafiti wake aliteua tamthilia nne, tamthilia ya *Pango* ikiwa mojawapo. Utafiti wake hata kama hauhusiani moja kwa moja na utafiti huu utatusaidia kuelewa sifa za mhusika mkuu wa kike ambaye ni Katango. Katika utafiti huu tutaangazia suala la utoupole na namna linavyochangia kukuza sifa za wahusika. Kwa hivyo tutachangiziwa kimawazo na utafiti wa Nyangweso.

Muniu (2013) alitafiti suala la ujinga wa mwanamke katika tamthilia ya *Pango*. Alitumia nadharia ya ufeministi kama dira ya kumwongoza katika utafiti wake. Katika utafiti wake Muniu alijikita katika ujinga wa mhusika mkuu ambaye ni Katango katika tamthilia hii. Katika utafiti wake alibainisha kuwa kuna wahusika mbalimbali ambao wana mchango chanya katika kumkuza mhusika wa kike kama vile Mamake Katango, Susa na Sota. Kwa upande mwingine kuna wahusika ambao wanampinga mhusika wa kike kwa mfano: Kikubi, Mbabekzai, Ngwese na Seki. Utafiti wa Muniu una umuhimu katika utafiti huu kwa sababu utatusaidia kuwaelewa wahusika mbalimbali katika tamthilia hii pamoja na majukumu yao. Kwa kuwa kuwaelewa wahusika na lugha wanayoitumia wanapowarejelea wengine ndiyo msingi wa utafiti huu. Hata hivyo utafiti wa Muniu unatofautiana na utafiti huu kwa kuwa Muniu alijikita katika suala la ujinga wa mwanamke nasi tutajikita katika uchanganuzi wa suala la utoupole kama linavyojitokeza katika tamthilia hii.

1.9 MISINGI YA KINADHARIA

Nadharia ya utoupole iliasisiwa na Culpeper (1996). Nadharia hii ina misingi yake katika nadharia ya upole ya Brown na Levinson (1987). Katika utafiti huu tumeanza kwa kueleza kuhusu nadharia ya upole ili kuiwekea msingi nadharia ya utoupole.

1.9.1 DHANA YA USO

Brown na Levinson walibuni nadharia yao ya upole kwa kutumia dhana ya “uso”. Dhana ya uso ilielezwa na Goffman (1967). Kulingana na Goffman (1967) uso ni thamani chanya ya kijamii ambayo mtu hujipa au hupewa kulingana na mtazamo ambao watu wengine huchukulia kuwa anauegemea katika mtagusano fulani wa kijamii. Goffman (1967) anaendelea kusema kuwa kuhifadhi uso humfanya mtu kuhisi vizuri kwa sababu mtu ana uhusiano wa kihisia na uso ambao anautunza katika hali mbalimbali za kijamii. Vile vile, kupoteza uso huwa na maana ya kupotea kwa mhimili ambao huhifadhiwa katika hali ya kijamii.

Kwa kuwa uso ni kitu hafifu, mtu anaweza akapoteza uso au akauhifadhi katika hali za kijamii. Katika mitagusano ya kijamii mzungumzaji hushiriki katika vitendo vya kuokoa uso wake na wa wasikilizaji wake. Kwa mujibu wa Bousfield (2008) ni kwamba kanuni ya uso ni sehemu muhimu sana katika nadharia ya upole ya Brown na Levinson na nadharia ya utoupole ya Culpeper Jonathan. Brown na Levinson (1987) walitumia dhana ya uso kubuni nadharia yao ya upole. Kulingana na dhana ya uso ni bia na kila binadamu anayo. Na kwamba kila binadamu ana aina mbili za uso: Uso chanya na uso hasi.

1.9.2 USO CHANYA NA USO HASI

Aina hizi za uso huelezwa kwa misingi ya matamania aliyonayo kila binadamu na hufanya juhudi kuhakikisha kuwa yanathaminiwa. Nyuso hizi hudokeza matamania tofauti katika maingiliano mbalimbali ya kijamii. Uso chanya hutamani mchango wake kutambuliwa, kuheshimiwa, kujumlishwa na kusifiwa nao uso hasi hutamani kuthaminiwa kuwa na uhuru wa kutenda anavyotaka binadamu kwa mfano: kutoshuriwa, kutoagizwa, kutoombwaombwa, kutotembelewa bila hiari yake, kwa ujumla hautaki kusumbuliwa. Kwa ujumla uso hasi ni tamania la kutaka kujiwekea mipaka ya uhuru wa kutoingiliwa.

Kwa kawaida katika kila mwingiliano mtu hutaka aina hizi za uso kuhifadhiwa lakini wakati mwingine kauli za msemaji huenda kinyume na matarajio haya. Hali hii inapotokea husababisha

vitendo vinavyotishia uso wa mzungumzaji na msikilizaji. Kwa kuwa uso ni kitu hafifu ni lazima uzingatiwe katika kila mwingiliano. Katika tukio la mawasiliano uso unaweza ukajengwa au kuumbuliwa. Hivyo basi kila mara mzungumzaji anapokabiliwa na hali zinazotishia uso ni lazima awe katika nafasi ya kuokoa uso wake na uso wa msikilizaji wake.

1.9.3 NADHARIA YA UPOLE

Brown na Levinson (1987) walibuni nadharia yao ya upole wakitumia dhana ya uso. Wanasema kuwa ipo mikakati minne ambayo huweza kutumiwa ili kuokoa uso wakati wa mawasiliano ambayo ni pamoja na: Mkakati ndani ya rekodi, Mkakati nje ya rekodi, Mkakati chanya wa upole na Mkakati hasi wa upole. Mikakati hii aghalabu hutumiwa ili kukabiliana na hali zinazotishia kudhuru uso wa msemaji na msikilizaji. Mkakati ndani ya rekodi hutumia kauli za moja kwa moja ambazo hazina utata wowote. Hulenga ujumbe bila ya kuhifadhi uso wa msikilizaji. Hufuata kanuni za ushirikiano kama zilivyoelezwa na Grice (1975) hasa kanuni ya namna. Aghalabu mkakati huu hutumiwa wakati ambapo watu ambao wamezoeana wanazungumza au wana uhusiano wa karibu. Watu hawa ni pamoja na: watu wa familia moja, marafiki au wanaofanya kazi pamoja. Pia huweza kutumiwa wakati wa dharura na kuna haja ya kutoa msaada. Kwa mfano: Usivuke njia kuna gari linakuja! Katika hali hii msemaji huwasilisha ujumbe bila ya kutilia maanani suala la uso.

Mkakati nje ya rekodi huwa hautumii kauli za moja kwa moja. Msemaji hufanya juhudi za kutohasiri uso wa msikilizaji wake kwa kutosema jambo moja kwa moja na wakati huo huo kuongea kwa namna ya kumwelekeza msikilizaji kuwa anatakiwa afanye jambo fulani. Katika mkakati huu msemaji hudokeza jambo na kumwacha msikilizaji kufasiri atakavyo. Mkakati huu hulenga kuokoa uso wa msikilizaji na msemaji. Kwa mfano msemaji anapotumia methali katika mazungumzo. Brown na Levinson (1987) wanasema kuwa mkakati huu unapotumika ujumbe huwa katika hatari ya kufasiriwa visivyo kwa kuwa si rahisi kuhusisha lengo moja wazi katika usemi husika. Mkakati huu huvunja kanuni za Grice (1975) hasa kanuni ya namna. Kwa hivyo humwacha msikilizaji kufasiri maana ya implikecha katika mazungumzo. Kwa mujibu wa mkakati huu ni kwamba msikilizaji hutarajiwa kuwa na elimuawali au uelewa wa kile ambacho kinalengwa kusemwa na mzungumzaji hasa kwa kurejelea kwa kina vidokezi katika kauli ya msemaji. Mkakati huu huzua utata kutokana na fasiri mbalimbali ambazo zinaweza kuhusishwa na kauli fulani. Kwa mfano badala ya kuagiza maji moja kwa moja wakati ambapo msemaji ana

kiu anaweza kutumia kauli kama vile: Mwenzangu kuna joto, na hali kama hii humfanya mtu huhisi kunywa maji.

Mkakati chanya wa upole hutumiwa ili kuokoa uso chanya wa msikilizaji hasa tamanio lake kuwa mahitaji yake yanashughulikiwa. Aghalabu mkakati huu hulenga kuusifu au wakati mwingine kuufurahisha uso chanya wa msikilizaji kabla ya kufanya vitendo usemi. Msemaji hujaribu kuashiria kuwa yeye na msikilizaji ni washiriki katika jambo fulani. Mkakati huu hudhihirisha hali ya kuwa pamoja kati ya msikilizaji na msemaji. Kwa hivyo mzungumzaji hufanya juhudi ya kuibua na kupalilia mazingira yanayodumisha mahusiano mema baina yake na msikilizaji katika mazungumzo. Mkakati chanya wa upole unaingiliana na mawazo ya Lakoff (1973) anayesema kuwa jukumu kuu la washiriki katika mchakato mzima wa mawasiliano ni kudumisha mazingira ya uwiano na kujaribu kuepuka hali zinazoweza kuvunja mawasiliano na kuwa kudumisha mawasiliano ni muhimu kuliko kuzingatia upole. Kwa mfano mkakati huu huweza kutumia mbinu kama vile kumsifu msikilizaji na kumwonyesha kuwa unamjali. Kwa mfano: msemaji anapotumia kauli kama vile: Hongera kaka kwa kununua gari jipya. Bila shaka litakufaa sana katika eneo ulilohamia.

Mkakati hasi wa upole nao hutumiwa na msemaji wakati ambapo anataka kitu kutoka kwa msikilizaji au kuingilia mambo ya ndani ya msikilizaji na wakati huo huo anazingatia kwamba ana uhuru wa kukataa. Aghalabu mkakati huu hutumiwa pale ambapo msemaji anahisi kuwa anamsumbua msikilizaji wake. Katika makakati huu msemaji hujaribu kupunguza makali na hali zinazoweza kutishia uso wa msikilizaji. Msemaji huwa na ufahamu kuwa ombi lake huenda likamkasirisha msikilizaji wake au hata likazua aibu na hivyo basi hujaribu kuepuka kuwasilisha matamano yake kwa njia ya moja kwa moja. Kwa mfano msemaji anaweza akatumia kauli kama vile: Samahani kwa kukusumbua dada Rehema, unaweza ukanikalia na hawa watoto nikimbie sokoni kununua mboga.

Kulingana na Brown na Levinson (1987), mikakati ya upole hubuniwa ili kuepuka kudhuru uso wa msemaji na msikilizaji. Kwa mujibu wa wataalamu hawa ni kuwa uso ni heshima ambayo mtu binafsi huwa nayo na hutarajiwa kudumishwa na wengine katika miktadha ya umma na kibinafsi. Kwa upande mwingine kulingana na Culpeper (1996), utoupole hutumiwa wakati ambapo msemaji huwa na lengo la kudhuru uso wa msikilizaji. Utoupole huhusisha vitendo vinavyohasiri uso vinavyotendwa kimakusudi na msemaji kwa lengo la kudhuru uso wa

msikilizaji ili kusababisha migongano ya kijamii na kuvunja mawasiliano. Vitendo hivyo ni kama vile: kuamuru, kuingilia faragha ya msikilizaji, kushauri, kumtusi msikilizaji miongoni mwa vingine.

1.9.4 NADHARIA YA UTOUPOLE

Kulingana na Culpeper (1996) hali ya utoupole hutokea katika muktadha ambamo msemaji anatenda vitendo vinavyohasiri uso wa msikilizaji kimakusudi ili kusababisha kutoelewana baina yao na kusababisha migongano ambayo huvunja mawasiliano baina yao. Hapa Culpeper anatofautiana na Brown na Levinson (1987) wanaosema kuwa msemaji na msikilizaji hushiriki katika vitendo vinavyoookoa uso wanapowasiliana. Culpeper (2005) anaeleza kuwa utoupole hutokea wakati ambapo msemaji anatenda kimakusudi vitendo vinavyodhuru uso wa msikilizaji au wakati ambapo msikilizaji anatambua kitendo cha msemaji kinanua kuhasiri uso wake au yote mawili. Mullary (2008) anazingatia sehemu ya pili ya ufafanuzi huu na kusema kuwa katika ufafanuzi huu jukumu la msikilizaji na pia lengo la vitendo usemi limezingatiwa. Yaani matendo ya kudhuru uso yanaweza kutokea kutegemea lengo la msemaji lakini msikilizaji asifasiri kama yenye kudhuru uso au vilevile msemaji, lengo lake linaweza kuwa si kudhuru uso lakini msikilizaji akafasiri kama yenye kudhuru uso. Kwa hivyo basi utoupole unaweza kufasiriwa kupitia mtagusano na unahitaji diskosi zinazotumiwa katika mtagusano huo kuchanganuliwa na msemaji na msikilizaji. Culpeper (1996) alibuni mikakati mitano ya utoupole ambayo ni pamoja na: Mkakati hasi wa utoupole, mkakati chanya wa utoupole, mkakati ndani ya rekodi wa utoupole, matumizi ya kejeli na kutowasilisha chochote.

1.9.4.1 Mkakati hasi wa utoupole

Kulingana na Culpeper (1996), mkakati huu hukusudiwa kudhuru uso hasi wa msikilizaji. Katika mkakati huu mzungumzaji huzidisha makali na hali zinazotishia uso wa msikilizaji wake. Katika mkakati huu msemaji huwa na ufahamu kuwa kauli zake huenda zikamkasirisha msikilizaji wake au hata zikazua aibu. Kupitia mkakati huu mzungumzaji hupita mipaka na kuingilia uhuru wa msikilizaji wake. Mbinu zinazotumiwa katika mkakati huu ni pamoja na: mzungumzaji kumrejelea msikilizaji kwa njia hasi, kuingilia faragha ya msikilizaji na kumdhalilisha msikilizaji wake. Kwa mfano:

- 1.Seki: Ushirikina gani? (*Kwa hasira*) Imani zetu; roho ya kuwepo kwetu; uboho wa mifupa yetu ya jamii ndio unauita ushirikina? Wewe tangu ugonee kupashwa...

Mama: Ahh... Hapana; usiyaleta hayo (*akiwaashiria Susa na Sota*) mbele ya watoto!

uk. 19

Katika mfano wa 1, Seki ambaye ni babake Katango anaingilia faragha ya Katango kwa kumwambia kuwa elimu aliyoipata ilikuwa imemkengeusha hadi akakataa kupashwa tohara. Katika jamii ya Seki ilikuwa desturi kwa msichana kukeketwa kila alipobaleghe. Maneno yake yanakusudia kudhuru uso hasi wa Katango hasa tamanio la kutotaka kuingiliwa.

1.9.4.2 Mkakati chanya wa utoupole

Kwa mujibu wa Culpeper (1996), Mkakati huu hukusudiwa kudhuru uso chanya wa msikilizaji hasa matamanio ya msikilizaji ya kutaka kukubaliwa katika jamii. Mbinu zinazotumiwa ni pamoja na: mzungumzaji kumpuuza msikilizaji wake, mzungumzaji kutumia maneno ya miiko katika mazungumzo, mzungumzaji kutomwonea msikilizaji huruma, msemaji kutafuta kutokubaliana na msikilizaji wake, msemaji kumtusi msikilizaji wake na mzungumzaji kutotaka kujihusisha na msikilizaji wake. Kwa mfano:

2. Mtu 1: Sikiliza kirukanjia wewe! Tangu leo, ukome, unasikia? Usijitie kumpinga mzee. Kigoda cha Pango hawezi kukalia mwanamke, unasikia? Hilo halijawahi kutokea katika historia ya huku kwetu na halianzi nawe, unasikia? (*Katango anajivuta kwa maumivu*)

Katango: Unaniumiza! Uk32

Katika mfano wa 2, Mtu 1 anadhuru uso chanya wa Katango kwa kumtusi kwa kumwita kirukanjia. Mtu 1 anatumia mkakati chanya wa utoupole hasa matumizi ya lugha ya matusi.

1.9.4.3 Mkakati ndani ya rekodi wa utoupole

Kulingana na Culpeper (1996), Mkakati huu hutumiwa katika hali ambapo msemaji anakusudia kudhuru uso wa msikilizaji wake. Msemaji hutumia kauli za dhahiri na zenye maneno machache sana. Kauli za msemaji huwa hazina utata wowote. Mkakati huu huzingatia kanuni za ushirikiano kama zilivyopendekezwa na Grice (1975) hasa kanuni ya namna. Katika mkakati huu uso hautiliwi maanani na vitendo vya kutishia uso hutendwa moja kwa moja. Hali hii inajitokeza katika mfano huu:

3. Sakina: Ndiyo lakini ulifanya kosa kuwanyima maji. Watu huishi kwa udugu ati!

Ngwese: Unanilaumu sasa?

Katika mfano wa 3, kauli za Sakina kwa Ngwese ni za moja kwa moja. Sakina anatumia kauli wazi ili kuupitisha ujumbe wake kwa njia wazi. Hapa anamweleza Ngwese wazi kuwa alifanya kosa la kuwanyima Susa na Sota ruhusu ya kuchota maji kisimani kwa kusema kuwa ile ardhi ya kisima ilikuwa yake. Na hivyo aliizungushia ua. Kwa hivyo, katika mfano huu Sakina anatumia mkakati wa ndani ya rekodi wa utoupole kuupujua uso wa Ngwese.

1.9.4.4 Matumizi ya kejeli au Mkakati nje ya rekodi

Kulingana na Culpeper (1996) mkakati huu humfanya msemaji kuonekana kuwa mpole kwa msikilizaji ilhali katika hali halisi huwa hajakusudia kuonyesha upole wowote kwa msikilizaji wake. Vitendo vinavyodhuru uso hutendwa kwa kutumia implikecha. Huhusisha matumizi ya implikecha ambapo msemaji huwasilisha ujumbe ulio kinyume na aliokusudia kuwasilisha kwa msikilizaji wake. Kwa hivyo ili msikilizaji kuweza kuelewa kitendo kama chenye utoupole huhitajika kufasiri implikecha inayohusika. Ufasiri huu huhitaji uelewa wa kina wa muktadha na lengo la msemaji. Kwa mfano:

4. Katango: Shhh nini? Unyama gani huu? Una hisia wewe?

Mtu II: (*Akicheka kwa dharau*) Aahh, unaogopa nini Katango? Iweje anayetaka kuwa mlinzi wa Pango awe mwoga kiasi hiki? (*Akitikisa kichwa kwa kutoamini*) Shh... shhh... Pango litaongozwa na mwoga hili? Jama tutapona? Uk.31

Katika mfano wa 4, Mtu II anamwuliza Katango anachoogopa kwa kutumia swali la balagha, ilhali ni wazi kuwa walikuwa wametumwa na Ngwese mpinzani wa Katango kisiasa kuwavamia Katango na Kibwana njiani ili kuwapiga na kuwajeruhi ili kumfanya Katango aghairi nia yake kisiasa. Kwa hivyo hisia za Mtu II za kuonyesha kumjali Katango si halali. Katika hali hii Mtu II anatumia mkakati wa utoupole wa kutumia kejeli kuuhasiri uso wa Katango.

1.9.4.5 Kutowasilisha chochote

Kulingana na Culpeper (1996) mkakati huu wa utoupole huhusu kuwa kimya wakati ambapo upole unatarajiwa katika desturi ya jamii. Kwa mfano mtu kupokea hisani kutoka kwa mtu

fulani kisha kutoshukuru au kutojibu salamu. Katika hali ya kawaida ni kwamba baada ya kupokea hisani kutoka kwa mtu fulani mtu hutarajiwa kushukuru. Kitendo cha kutoshukuru hufasiriwa kama chenye utoupole kwani huvuruga uhusiano baina ya wahusika. Vile vile kila mara mtu akiamkuliwa hutarajiwa kujibu salamu. Kutojibu salamu huvuruga utaratibu wa jamii. Pia kitendo cha mtu kuondoka bila ya kusema kwaheri hufasiriwa kama chenye utoupole. Kwa mfano:

5. Kikubi: Aisee vipi?

(Kibwana amezama tu kwenye gazeti hajibu)

Kikubi: *(Akimwinamia)* Hellooo! *Mister*, gazeti linasema ulimwengu utaisha lini?

Uk.24

Katika mfano wa 5, mazungumzo haya yanatokea katika mkahawa wa Kauleni ambapo Mbabekazi na Kikubi wanaingia na kumkuta Kibwana amezama katika kusoma gazeti. Kikubi anamsalimu lakini Kibwana hajibu anaendelea tu kusoma gazeti. Hapa Kibwana anatumia mkakati wa utoupole wa kutowasilisha chochote kuupujua uso wa Kikubi. Kwani katika hali ya kawaida hutarajiwa kuwa mtu anaposalimiwa ajibu salamu. Kutojibu salamu hufasiriwa kama kitendo cha utovu wa nidhamu katika jamii nyingi ulimwenguni.

1.0.1 MBINU ZA UTAFITI

Katika sehemu hii tutafafanua kwa kifupi namna tutakavyoteua sampuli, kukusanya data, kuchanganua data na kuwasilisha matokeo ya data yetu.

1.0.2 Uteuzi wa sampuli

Katika utafiti huu tulitumia sampuli lengwa ambayo ni tamthilia ya *Pango*. Mbinu ambayo ilitumika kuteua sampuli hii ni uteuzi wa kimakusudi. Katika mbinu hii mtafiti mwenyewe kwa hiari yake huamua kuchagua kundi la watu au vitu ambavyo anaamini kwamba vinaweza kumpatia data itakayofanikisha malengo ya utafiti wake. Kwa hivyo tulichagua tamthilia hii ya *Pango* kwa kuwa tuliamini kuwa ingetusaidia kupata habari za kina kuhusu suala la utoupole tulilolichunguza. Katika utafiti huu mtafiti alitumia tamthilia kama sampuli lengwa kwa sababu tamthilia huhusisha lugha ya mazungumzo kwa njia ya moja kwa moja. Kwa hivyo ilikuwa

rahisi kwa mtafiti kuchanganua namna mikakati ya utoupole inavyotumiwa na wahusika kuhasiri uso wa wenzao katika mazungumzo na kusababisha uhasama miongoni mwao.

1.0.3 Mbinu za kukusanya data

Katika utafiti huu data ya kimsingi ilitoka katika tamthilia ya *Pango*. Ili kubainisha namna wahusika wanatumia mikakati mbalimbali ya utoupole kudhuru uso wa wenzao katika mazungumzo, tamthilia ya *Pango* ilitumiwa katika uchunguzi. Tamthilia ya *Pango* ilitumiwa kimakusudi ili kupata data iliyofanikisha uchunguzi huu. Baada ya kuisoma tamthilia hii mara kadhaa, kauli zote za wahusika zilizofikiriwa kuwa zenye utoupole zilinakiliwa ili kufanikisha uchunguzi wa mikakati ya utoupole inavyotumiwa na wahusika kuhasiri uso wa wenzao katika mazungumzo.

Pia mtafiti alisoma vitabu, majarida, tasnifu na makala nyinginezo zinazohusiana na mada hii ya utafiti na nadharia ya utoupole. Katika nadharia ya utoupole mtafiti alizingatia mikakati ya utoupole ambayo ni pamoja na: mikakati ya utoupole chanya, mikakati ya utoupole hasi, mikakati ya ndani ya rekodi ya utoupole, matumizi ya kejeli na mikakati wa kutowasilisha chochote.

1.0.4 Uchanganuzi wa data

Baada ya mtafiti kunakili kauli za wahusika zilizofikiriwa kuwa zenye utoupole, aliziainisha kulingana na mikakati ya utoupole ambayo ni pamoja na utoupole hasi, utoupole chanya, matumizi ya kejeli, kutowasilisha chochote na mikakati ndani ya rekodi. Halafu ikafafanuliwa kwa misingi ya malengo ya utafiti huu pamoja na mihimili ya nadharia ya utoupole kama ilivyoelezwa na Culpeper (1996). Kisha tulichanganua pia ambavyo mikakati ya utoupole inachangia katika kuzikuza sifa za wahusika na kuenedeleza maudhui katika tamthilia ya *Pango*.

1.0.5 Uwasilishaji wa matokeo ya data

Baada ya mtafiti kukusanya na kuchanganua data, data hii ilitusaidia katika kuyafikia madhumuni ya utafiti huu pamoja na kujibu maswali ya utafiti huu. Mtafiti aliwasilisha matokeo yake kwa kutumia njia ya ripoti ambayo ndiyo tasnifu yenyewe. Mtafiti alieleza namna kauli za wahusika ambazo zimetumia mikakati ya utoupole zilichangia kuzikuza sifa zao na kuenedeleza maudhui katika tamthilia ya *Pango*.

SURA YA PILI

MATUMIZI YA MIKAKATI YA UTOUPOLE KATIKA TAMTHILIA YA *PANGO*

2.1 UTANGULIZI

Katika sehemu hii, tutabainisha namna wahusika katika tamthilia ya *Pango* wameitumia mikakati mbalimbali ya utoupole. Tamthilia hii ilituliwa kimakusudi ili iweze kutupa data ambayo itafanikisha malengo ya utafiti huu. Kauli za wahusika katika tamthilia ya *Pango* zinazoashiria utoupole zimechanganyuliwa kwa msingi wa nadharia ya utoupole ya Culpeper (1996).

Mikakati ya utoupole ambayo imetumiwa na wahusika katika tamthilia teule pamoja na kategoria zake zinazotumiwa kudhuru uso imejadiliwa na kutolewa mifano faafu kutoka katika tamthilia teule. Vile vile, tutachunguza namna suala la kidrama linabainika kupitia mikakati mbalimbali ya utoupole inayotumiwa na wahusika katika tamthilia hii. Kwa kutekeleza hili kazi hii imechunguza mikakati mitano ya utoupole katika nadharia ya utoupole ya Culpeper (1996). Mikakati hii ya utoupole inayoshughulikiwa katika sehemu hii ni pamoja na: Mikakati hasi wa utoupole, mikakati chanya wa utoupole, mikakati ndani ya rekodi wa utoupole, matumizi ya kejeli na kutowasilisha chochote.

2.2 Sinopsia ya tamthilia ya *Pango*

Pango (2003) ni tamthilia ya pili ya Wamitila baada ya tamthilia yake ya *Wingu la Kupita* (1999). Anwani ya tamthilia hii ina maana kadha, kwanza ni jina la mahali katika nchi ya Chemwa. Pili pango ni mahali palipoheshimiwa kwani mizimu iliishi mahali hapa. Ndiyo maana hata watoto hawakuruhusiwa kupachezea mahali hapo kwa sababu wakazi waliamini kuwa huenda mizimu ikahamaki na kuwadhuru. Tatu pango palikuwa mahali pa kutolea kafara. Tamthilia ya *Pango* imegawika katika sehemu tatu. Sehemu ya kwanza ina maonyesho matano, sehemu ya pili ina maonyesho matatu nayo sehemu ya tatu ina maonyesho manne.

Tamthilia inaanza kwa Ngwese kuwakataza Susa na Sota kuteka maji akidai kuwa ardhi iliyokuwa na kisima ni yake na amezungushia ua ili kuwazuia watu kuikanyaga. Watoto hawa wanamrai Ngwese awaruhusu kuteka maji lakini anakataa katakata. Kelele baina yao inasababisha Sakina kuja na kutaka kujua chanzo cha kelele hizo. Anapojua kiini chake anamweleza Ngwese kuwa angewaruhusu watoto kuteka maji. Ngwese anakerwa zaidi na kauli

ya Sakina na anamwamuru aondoke pale. Sakina anaondoka na kumwacha mzee Ngwese akijizungumzia.

Kisa cha Katango na Ngwese kukutana kinafuata. Mazungumzo yanayotokea kati yao yanadhihirisha kuwa kuna uadui wa kisiasa baina yao. Katango anamweleza Ngwese kuhusu alivyomwona akiwafukuza Susa na Sota kama ndege walipokuwa wameenda kisimani kuteka maji. Ngwese anakana madai haya na kusema ati huo ni uzushi tu wa Katango. Katika mazungumzo yanayofuata inabainika kuwa Ngwese anatawaliwa na taasubi za kiume kwa mfano anamweleza Katango kwamba mwanamke ni mwanamke tu awe na elimu au la katika ukurasa wa 10. Tukio hili linamtia msomaji hamu ya kutaka kusoma zaidi ili aelewe Katango atakavyokabiliana na kitendo hiki kinachohasiri uso wake. Ngwese anamfahamisha Katango kuhusu nia yake ya kuwania kuwa kiongozi wa Pango. Naye Katango pia anamweleza kuhusu azma yake ya kutaka kuwa kiongozi wa Pango. Hiki ndicho kiini cha ushindani baina yao na ndio mgogoro mkuu wa tamthilia nzima.

Watoto wanarudi nyumbani wakiwa wamechelewa kutoka kisimani. Wanapofika nyumbani wanamweleza mama yao chanzo cha kuchelewa kwao. Katango anaingia na kukubaliana na sababu za kuchelewa kwao. Seki anamtetea sana Ngwese kwa kusema kuwa kuchelewa kwa kina Susa na Sota kulitokana na wao kuchezea pangoni. Katango anamweleza Seki nia yake ya kutaka kuwa kiongozi wa Pango, lakini Seki anamvunja moyo bintiye badala ya kumtia shime aendelee na azma hiyo. Ukengeushi wa Katango wa kubeba mshale na mata unasababisha mgogoro mkali baina yake na Seki. Seki anamweleza kuwa kulingana na utamaduni wao wanawake hawakuruhusiwa kubeba vitu hivi. Pia anamweleza Katango alivyokwenda kinyume na utamaduni wao kwa kugomea kupashwa tohara. Kulingana na elimu ya Katango ni kwamba mambo yamebadilika na vitendo hivyo havina maana katika jamii ya sasa kwani vimepitwa na wakati.

Kisa kinachofuata kinatukia katika mkahawa wa Kauleni ambapo vijana wanajadiliana kuhusu habari walizoziona katika gazeti kuhusu Katango kuwania uongozi wa Pango. Kunaibuka mjadala mkali kati ya wanaomuunga mkono na wanaompinga. Ghafla Katango anawasili pale hotelini na nduguze ambao ni Susa na Sota. Anaingilia mjadala unaoendelea na kutetea sababu zake za kutaka kuwa kiongozi. Inasadifu kuwa hata Ngwese na wafuasi wake wawili wanaingia

mkahawani na kuanzisha mazungumzo na Kauleni. Katango anapomwona Ngwese pale mkahawani anaondoka bila ya kuonana naye.

Baada ya Katango kuondoka hotelini akiwa na Kibwana, wanashambuliwa na watu wawili. Ghafila Susa na Sota wanajitokeza na kumpiga mmoja wa watu hao kwa yai na kukomesha vita baina yao. Hadithi inabadilika kwa kasi na kutupeleka ambapo tunaona kundi la vijana likimbeba Katango huku likiimba nyimbo zinazomsifu. Pia kundi la pili linatokea likiwa limembeba Ngwese huku likiimba nyimbo za kumsifu. Ghafila Babu anatokea na kuyaongoza makundi haya mawili kwa kumpa nafasi kila mmoja ya kujitetea mbele ya umati. Katango alipewa nafasi ya kwanza kisha Ngwese. Kila mmoja alifanya juu chini kujitetea na halafu uchaguzi ukafanywa ambapo Ngwese anamshinda Katango vibaya sana.

Uchaguzi unapokamilika, kila mmoja anarudi nyumbani. Katika makao ya Ngwese tunakutana na Sakina akimhiza Ngwese aende kazini. Ngwese kwa upande wake anaendelea kulisoma gazeti lenye habari za ushindi wake. Ngoi na Kauleni wanaingia nyumbani kwa Ngwese na kuusifia ushindi wake. Naye Katango alikuwa nyumbani kwao akiomboleza ushinde wake huku akiliwazwa na wazazi wake. Kibwana na Kikubi wanaingia na kumfahamisha Katango kuhusu mchezo unaochezwa pangoni na Susa na Sota.

Katango, Kibwana na Kikubi wanafunga safari kuelekea pangoni kuhakikisha kuwa ni Susa na Sota ndio wachezeao mle pangoni. Katika sehemu inayofuata tunapatana na mtu akiwa amelala pangoni huku akijizungumzia. Ghafila Susa na Sota wanaingia na kubaini kuwa yule ni Katango ambaye ni dada yao. Wanaamua kwenda kumjuvya baba yao kuhusu anayechezea pangoni. Pia wanamweleza kuhusu alivyokuwa haongei na alivyojaribu kutoroka ila akashindwa.

Seki anatokea na kushikilia kuwa waliochezea pangoni ni Sota na Susa na hivyo wakamfanya akaaye pangoni kulalamika. Susa na Sota wanamweleza Seki kuwa ni Katango ndiye anayechezea pangoni. Seki anafurahishwa na hili kisha Katango anaingia na kukaa bila ya kuongea halafu anaondoka.

Susa na Sota wakiwa mbele ya pango wanasikia sauti ikitoka pangoni. Mara wanaona sarafu na kijikaratasi chenye maandishi ya ajabu. Kijikaratasi kimoja kiliandikwa maneno mawili kwa herufi kubwa ambayo ni: pauni na dola, nacho kingine kiliandikwa kwa herufi ndogo maneno ambayo yalikuwa ni yuro na yen. Kisha sauti inasikika na kuongea juu ya maua na asali.

Hatimaye Susa na Sota wanapanga kwenda kumfahamisha baba yao kwamba walimwona aliyevuruga pango. Isipokuwa walihofia kuwa huenda baba yao akakosa kuwaamini.

Mwishoni mwa tamthilia majitu matatu yanashuhudiwa ambayo yamejifunika maguo meusi ili yasionekane. Kinyume cha matarajio ni kwamba miongoni mwa haya majitu walikuwemo Ngwese, Seki na vibaraka wake ambao wanashikwa pangoni pale na kikosi kilichoongozwa na Katango kwa sababu walishiriki ufiadini. Kabla ya tukio hili Ngwese na Seki waliwalaumu wengine kwa kuchezea pangoni. Mama pamoja na wanawake wengine hata vijana na wazee wanaungana na Katango kuelekea pangoni ambapo Ngwese na vibaraka wake wanashikwa na polisi. Hili linaashiria kuporomoka kwa utawala wa Ngwese na huu unakuwa mwanzo wa utawala wa vijana unaoongozwa na Katango. Wanajamii wote wanafurahi na kusherehekea ushindi huu.

2.3 Matumizi ya Mkakati Hasi wa Utoupole

Kulingana na Culpeper (1996), mkakati huu hukusudiwa kudhuru uso hasi wa msikilizaji. Katika mkakati huu mzungumzaji huzidisha makali na hali zinazotishia uso wa msikilizaji wake. Katika mkakati huu msemaji huwa na ufahamu kuwa kauli zake huenda zikamkasirisha msikilizaji wake au hata zikazua aibu. Kupitia mkakati huu mzungumzaji hupita mipaka na kuingilia uhuru wa msikilizaji wake. Mbinu zinazotumiwa katika mkakati huu ni pamoja na: mzungumzaji kumrejelea msikilizaji kwa njia hasi, msemaji kuingilia faragha ya msikilizaji, mzungumzaji kumdhalilisha msikilizaji wake na mzungumzaji kumtisha msikilizaji wake.

2.3.1 Mzungumzaji Kumrejelea Msikilizaji kwa Njia Hasi

Katika tamthilia teule kuna hali mbalimbali ambazo mhusika mmoja anamhusisha mwenzake na uhasi fulani ili kuvunja mazungumzo baina yao. Kwa mfano:

6. Ngwese: ... Huna chochote cha kunitisha isipokuwa huo mdomo mrefu tu na
kama hujui mwenye kinywa kirefu hujichoma mwenyewe. Nitakuwa
kiongozi ... utaona tu! Utaona, nakwambia!

(mtuo)

Najua kinachokusumbua. Nakielewa kinachowasumbua watu kama wewe?

Katango: Unakijua ehh?

Ngwese: Ndiyo unasumbuliwa na wivu! Uk.12

Katika mfano wa 6, mazungumzo haya yanatokea baina ya Katango na Ngwese wanapokutana njiani asubuhi moja. Ngwese anamweleza Katango kuhusu nia yake ya kuwania uongozi wa pango. Katango pia anamweleza nia yake ya kuwania uongozi wa pango. Ndipo Ngwese anamweleza Katango kuwa hana chochote cha kumtisha. Ngwese anahasiri uso hasi wa Katango kwa kumhusisaha na uhasi. Kwani tabia ya kuwa na wivu ni tabia hasi na kawaida hakuna binadamu ambaye hutaka kuhusishwa nayo. Aidha Ngwese anamhusisha Katango na udaku anapomwambia kuwa ana mdomo mrefu. Hii pia ni tabia hasi ya kuhusishwa nayo.

7. Ngwese: Ahh, kisirani chenyewe hiki hasa! Babu alisema kukumbana na mwanamke asubuhi ni kisirani, siku nzima anaichafua. (*Kwa Katango*)
Mwanamke, unasaka nini hapa?

Katango: Je, unadhani ubabe wako unanitisha mimi? Mimi sio watoto unaowafukuza watakapo kuchota maji! Uk.10

Katika mfano wa 7, Ngwese anamhusisha Katango na tabia hasi. Katika hali hii, Ngwese anadhuru uso hasi wa Katango kwa kumhusisha na uhasi anapomwita kisirani. Kisirani ni mtu anayesababisha kuwepo kwa balaa au maafa. Aghalabu binadamu huwa hataki kuhusishwa na tabia hasi kama hii.

8. Seki: Nisiyalete vipi na unamwona kigego wako huyu ananikasirisha? (*Kimya*) Wote wanadanganya; hamna maji waliyonyimwa (*Kwa Susa na Sota na kwa sauti ya juu*) Nyie mkienda kucheza michezo yenu huko na kuchelewa msije kuzua zua hapa! Hii isiwe likizo ya kusema uongo!

Mama: Seki, mwenzangu hatuwezi kuwapuza. Uk.19

Katika mfano wa 8, Seki anazungumza na kumhusisha Katango na tabia hasi ya kigego. Kigego ni mtu mkorofi ambaye hafuati yale anayoambiwa. Katika hali ya kawaida katika jamii mtu huwa hapendi kuhusishwa na uhasi wowote katika jamii anamoishi. Hivyo basi, babake Katango anahasiri uso hasi wa Katango kwa kumwita kigego.

2.3.2 Mzungumzaji kuingilia faragha ya msikilizaji

Mbinu hii hutumiwa na mzungumzaji ili kuhasiri uso hasi wa msikilizaji wake. Aghalabu binadamu hujiwekea mipaka ya kutoingiliwa. Mzungumzaji anapoingilia faragha ya msikilizaji wake huwa na nia ya kuhasiri uso hasi wake. Katika tamthilia ya *Pango* kuna hali mbalimbali ambazo wahusika wanaingilia faragha za wenzao. Kwa mfano hali hii inajitokeza katika mifano ifuatayo:

9. Katango: ... Najua nini? Kwani unadhani yamefichwa na yatafichwaje? (*mtuo*) Nani asiyejua kuwa alikuwa kibarakala wa wakoloni?

Ngwese: Mwanamke we! Usinitusi!

Katango: Ni ukweli na unachonyota ngozini kama upupu. (*Mtuo*) Babu yako hakushirikiana na wakoloni kuwasaliti waliopigana kuikomboa jamii yetu hii?

Uk.12

Katika mfano wa 9, Katango anatumia makakati hasi wa utoupole anapoingilia faragha ya Ngwese kwa kuingilia familia yake hasa anapomwambia Ngwese kuwa babu yake alikuwa kibaraka wa wakoloni. Kwani alishirikiana nao na kuishia kuwasaliti waliopigana ili kuikomboa jamii yao. Kwa hivyo katika mfano huu Katango anahasiri uso hasi wa Ngwese hasa tamanio la uso hasi la kutotaka kuingiliwa.

10. Seki: Ushirikina gani? (*Kwa hasira*) Imani zetu; roho ya kuwepo kwetu; uboho wa mifupa ya jamii ndio unauita ushirikina? Wewe tangu ugomee kupashwa ...

Mama: Ahh... Hapana; usiyalete hayo (*akiwaashiria Susa na Sota*) mbele ya watoto!

Uk.19

Katika mfano wa 10, mazungumzo haya yanatokea baada ya Katango kuokota mata na mshale njiani. Baada ya Seki kumwona na vitu hivi anamwambia kuwa wanawake hawakuruhusiwa na utamaduni kuvibeba vitu hivi kwani kitendo kama hicho kingemletea mhusika balaa. Ndipo Katango anamwambia kuwa huo ni ushirikina. Naye babake kwa kutaka kuuhasiri uso hasi wa Katango anaingilia faragha yake kwa kumwambia kuwa aligomea kupashwa tohara. Kwa mujibu wa utamaduni wa jamii hii ni kuwa wanawake walipashwa tohara. Kwa hivyo Katango kukataa kupashwa tohara alichukuliwa kuwa mwasi wa utamaduni. Babake Katango anatumia mbinu ya

kuingilia faragha ya Katango ili kudhuru uso hasi wake hasa tamanio la kutotaka kuingiliwa. Na anafanya hivi hadharani mbele ya ndugu zake ili kumwaibisha au kumvunjia heshima Katango. Ndipo Mama anapomwambia mumewe kuwa asiyaleta hayo mbele ya kina Susa na Sota kwani kulingana naye masuala ya kitamaduni ni ya faraghani.

11. Polisi II: Mzee, tumekuja kukuchukua. Unatuhumiwa kufuja mali ya umma ulipokuwa mkurugenzi katika shirika la umma!

Ngwese: (*Akitikisa kichwa*) Ahh, hapana bwana wee! (*Kwa sauti*) Nyie mnajua mnacheza na nani? Hapana, haiwezekani! (*Akimwangalia Katango*) Huu ni uzushi tu wa kulipaka matope jina langu... uk. 87

Katika mfano wa 11, mazungumzo haya yanayojiri baada ya polisi wawili kutumwa na mamlaka ya juu nchini Chemwa kuja kumchukua Ngwese kwenda kujibu mashtaka yanayohusiana na ufisadi. Polisi II anahasiri uso hasi wa Ngwese kwa kuingilia faragha yake anapodai kuwa Ngwese alifuja mali ya umma alipokuwa mkurugenzi katika shirika fulani la umma.

2.3.3 Mzungumzaji Kumkebehi Msikilizaji Wake

Mbinu ya kutumia kebehi ni kategoria ya mkakati hasi wa utoupole. Katika matumizi ya mbinu hii mtu humwambia mwenzake maneno ya kumuudhi kwa utani au mzaha. Maneno haya huteuliwa kwa uangalifu mkubwa ili yaweze kumkasirisha msikilizaji wake. Maneno haya huwa makali katika sikio la msikilizaji wake na hutishia uso hasi wa msikilizaji. Kwa mfano:

12. Katango: Nataka kuwasimulia hadithi ...

Ngwese: (*Kwa dharau*) Hili sio darasa! Sisi sio watoto wa shuleni! Uk.42

Katika mfano wa 12, mazungumzo haya yanatokea katika uwanja wa kutolea hotuba ambapo Babu anaongoza na kuhakikisha kuwa kila mmoja anapewa fursa ya kueleza nia yake ya kuwania kuwa mlinzi wa pango. Katango ndiye anayepewa fursa ya kwanza na anaungwa mkono na wafuasi wake. Ili kuweza kuwavutia wafuasi wake anatumia mbinu ya kusimulia hadithi. Anapoanza kunena anasema kwamba anataka kusimulia hadithi ndipo Ngwese anamjibu kwa kebehi kuwa hili si darasa wala wao sio watoto wa shuleni. Hapa Ngwese anahasiri uso hasi wa Katango kwa kumwambia kimzaha maneno yanayonua kumkasirisha ili kumvunja Katango moyo wa kuendelea na usimulizi wake.

13. Katango: Mnataka nini?

Mtu I: (*Kwa dhihaka*) Tunakutaka wewe? Wewe mwenyewe hasa! (*Akimsogea*) Huoni raha, hivyo au tuseme hutaki kupendwa na ... (*anamshika*) kuguswa guswa...
uk.32

Katika mfano wa 13, mazungumzo haya yanayotokea kati ya wale watu waliotumwa na Ngwese kuwavamia Katango na Kibwana kwa lengo la kumfanya Katango aache kumpinga Ngwese kwa kuwania uongozi wa Pango. Watu hawa wanawajongea Katango na Kibwana kisha wanaanza kumgusagusa Katango. Ndipo Katango anapowauliza wanachokitaka halafu Mtu I anamjibu kwa kebehi kwamba wanamtaka Katango. Maneno ya Mtu I yanakusudia kuhasiri uso hasi wa Katango.

14. Katango: Ndiyo maana lazima ateuliwe kiongozi afaaye!

Seki: Na huyo kiongozi afaaye ni wewe sio?

Katika mfano wa 14, mazungumzo haya yanatokea baada ya Seki kumweleza Katango kuwa aache nia yake ya kuwania uongozi kwani huku ni kumpinga Ngwese katika azma yake ya kuwa kiongozi. Ndipo naye Katango anapomwambia kuwa bora kiongozi afaaye ateuliwe. Seki anamjibu kwa kebehi akitumia swali la balagha anapomwuliza kama huyo kiongozi afaaye ni yeye. Katika hali hii Seki anakusudia kuuhasiri uso hasi wa Katango kwa kutumia mbinu ya matumizi ya kebehi.

2.3.4 Mzungumzaji Kumtisha Msikilizaji Wake

Katika tamthilia ya *Pango* zipo hali kadhaa ambazo mzungumzaji anamtisha msikilizaji wake akiwa na nia ya kuhasiri uso hasi wake. Kwa mfano:

15. Ngwese: (*Anajaribu kumsogea kwa hasira*) Nitakupapata makofi wewe. Naona unanikosea adabu! Unatakiwa kuolewa, utiwe adabu na mumeo.

Katango: Huu wakati mwingine! Uk. 14

Katika mfano wa 15, Ngwese anakusudia kudhuru uso hasi wa Katango kwa kumtisha kuwa angempapata makofi. Kauli hii inalenga kumjaza Katango woga wa kuendelea kujibizana na Ngwese.

16. Seki: (*Kwa sauti ya kutisha*) Endeleeni kuchezecheza hapo mtajakumbwa na Subiani mjute kufanya machezo yenu hapo. (*Sota na Susa wanatazamana kwa woga. Baada ya muda wanaondoka kimya kimya kwenda mafugani. Katango anacheka akielekea upande wa pili huku ameshika ule uta na mata*)

Mama: Usiwatie watoto hofu ya bure... uk. 22

Katika mfano wa 16, Seki anahasiri uso hasi wa kina Susa na Sota kwa kuwatisha kuwa wakiendelea kuchezea pangoni wangepatwa na Subiani na kuishia kujutia kitendo chao.

2.4 Matumizi ya Mkakati Chanya wa Utoupole

Kwa mujibu wa Culpeper (1996), Mkakati huu hukusudiwa kudhuru uso chanya wa msikilizaji hasa matamano ya msikilizaji ya kutaka kukubaliwa kama sehemu ya kundi katika jamii. Mbinu zinazotumiwa ni pamoja na: mzungumzaji kutotaka kujihusisha na msikilizaji wake, mzungumzaji kumtusi msikilizaji wake, mzungumzaji kumpuuza msikilizaji wake, mzungumzaji kutumia maneno ya miiko katika mazungumzo, mzungumzaji kumpa msikilizaji utambulisho ambao haufai, mzungumzaji kutomwonea msikilizaji huruma na msemaji kutafuta kutokubaliana na msikilizaji wake.

2.4.1 Mzungumzaji Kutotaka Kujihusisha na Msikilizaji Wake

Katika tamthilia teule kuna hali ambazo mzungumzaji anatoa kauli zinazoonyesha kwamba hataki kujihusisha na msikilizaji wake. Katika mkakati huu msemaji hujaribu kuepuka kutumia kauli zote zinazoweza kuibua na kupalilia mazingira yanayodumisha mahusiano mema, na badala yake hutumia kauli zinazoweza kuvunja mazungumzo kati yake na msikilizaji wake. Kwa mfano:

17. Sota: Sisi hatuchezi pangoni!

Ngwese: (*Kwa hasira*) Ondokeni kabisa! Hapa hamtakiwi kabisa nyie! (*Sota na Susa wanaondoka mbio mbio. Sakina anaingia wakati huu*) Uk.6

Katika mfano wa 17, Ngwese anawafukuza Sota na Susa wanapoelekea kisimani kuteka maji ili wasikanyage ardhi yake ambayo tayari ameizungushia ua. Kauli ya Ngwese kwa kina Susa na Sota inadhihirisha kwamba Ngwese hataki uhusiano wowote nao. Ngwese anatumia mkakati chanya wa utoupole ili kudhuru uso chanya wa kina Sota na Susa hasa tamano la uso chanya wa

binadamu la kutaka kutambuliwa kama sehemu ya kundi fulani katika jamii. Ngwese anavunja uhusiano wake na Susa na Sota kwa kuwaambia kuwa waondoke hapo na kwamba hawakutakiwa katu mahali pale.

18. Sakina: Ni kosa ndiyo.

Ngwese: (*Akiashiria*) Kwanza wewe, rudi huko ulikokuwa! Unanitilia ukuba siku yangu wewe. Uk.7

Katika mfano wa 18, mazungumzo haya yanatokea baina ya Ngwese na Sakina. Hii ni baada ya Sakina kusikia Ngwese akiongea kwa sauti ya juu alipokuwa akiwakataza Susa na Sota kukanyaga ardhi yake. Sakina baada ya kuelewa alilofanya Ngwese anamweleza kuwa alilofanya ni kosa. Ndipo Ngwese anamwamuru Sakina kurudi alikokuwa. Pia anaongezea kuwa asimtilie nuksi katika siku yake. Ngwese anahasiri uso chanya wa Sakina kwa kukataa kujihusisha naye anapomwamuru kurejea alikotoka.

2.4.2 Mzungumzaji Kumtusi Msikilizaji Wake

Mbinu hii ya mkakati chanya wa utoupole inakinzana na kanuni za mawasiliano kama zilivyopendekezwa na Leech (1983) hasa kanuni ya msemaji kumsifu msikilizaji wake. Katika mbinu ya msemaji kumtusi msikilizaji wake, mzungumzaji hukuudia kuuhasiri uso chanya wa msikilizaji wake. Matumizi ya lugha ya matusi yanadhihirika katika hali kadha hasa yakiwa yamechochewa na tofauti za kimamlaka kati ya mzungumzaji na msikilizaji.

Kwa mujibu wa Culpeper (1996), suala la utoupole hutokea kwa wingi katika mawasiliano wakati ambapo msemaji ana mamlaka zaidi ya msikilizaji. Mawazo haya ya Culpeper yanaungwa mkono na Locher na Bousifield (2008) wanaposema kuwa dhana ya mamlaka ni muhimu sana wakati wa kujadili suala la utoupole katika mazungumzo. Mamlaka katika mazungumzo huhusu hadhi ya msemaji na msikilizaji, nguvu za kimwili au tabaka miongoni mwa masuala mengine. Wanasonga mbele kwa kusema kuwa katika hali ambapo msemaji ana mamlaka zaidi ya msikilizaji, mzungumzaji humdhibiti msikilizaji wake zaidi. Fauka ya haya, ni kwamba wanadai kuwa utoupole ni njia mojawapo ya msemaji kutumia madaraka aliyonayo. Mbinu ya msemaji kutumia lugha ya matusi inadhihirika katika hali zifuatazo. Kwa mfano:

19. Ngwese: Ni nini unachobwekea hapa?

Katango: Hayo nayo siyo matusi? Uk.13

Katika mfano wa 19, mazungumzo haya yanatokea baada ya Katango kumwambia Ngwese kuwa amepofushwa na ushirikina. Naye Ngwese anamwelezea Katango kwamba alikuwa ameenda kumtegea ndumba njiani ili ndoto yake ya kuwa mlinzi wa pango itibuke. Ndipo Ngwese anapomwuliza Katango kwa kutumia lugha ya matusi kile ambacho Katango alikuwa akibwekea. Hapa Ngwese anatumia mkakati chanya wa utoupole hasa matumizi ya lugha ya matusi katika mazungumzo kwa sababu ana mamlaka ya nguvu za kiuchumi zaidi ya Katango ambaye ni mwalimu. Hapa Ngwese anakusudia kuhasiri uso chanya wa Katango.

Katika mfano mwingine ni kuwa matumizi ya lugha ya matusi yanajitokeza katika hali hii ambapo Ngwese alikuwa amewatuma watu wawili kuwavamia Katango na Kibwana wakiwa njiani.

20. Mtu I: Sikiliza kirukanjia wewe! Tangu leo, ukome, unasikia? Usijitie kumpinga mzee. Kigoda cha Pango hawezi kukalia mwanamke, unasikia? Hilo halijawahi kutokea katika historia ya huku kwetu na halianzi nawe, unasikia? (*Katango anajivuta kwa maumivu*)

Katango: Unaniumiza! Uk32

Katika mfano wa 20, Mtu I anadhuru uso chanya wa Katango kwa kumtusi kwa kumwita kirukanjia. Matumizi haya ya lugha ya matusi yanachochea na hali kwamba hawa watu waliotumwa na Ngwese wana nguvu za kimwili zaidi ya Katango. Mtu I anatumia mkakati chanya wa utoupole hasa matumizi ya lugha ya matusi ili kudhuru uso chanya wa Katango.

2.4.3 Mzungumzaji Kutumia Maneno ya Miiko Katika Mazungumzo

Katika tamthilia ya *Pango*, kuna hali ambazo mzungumzaji anatumia maneno ya miiko katika mazungumzo. Maneno ya mwiko ni yale maneno ambayo jamii imeyafungia matumizi yake kwa vigezo mahususi vya kitamaduni. Maneno mwiko yanapotumiwa huwa na nia ya kuibua hisia mbaya kwa msikilizaji wake. Aghalabu katika jamii nyingi watu hukwepa kuzungumzia mada ambazo ni mwiko. Mara nyingi mada zilizo za mwiko zinapozungumziwa huwaudhi wasikilizaji wake. Maneno mwiko huamuriwa na utamaduni na jamii. Neno huchukuliwa kuwa mwiko pale

ambapo linafikiriwa kuwa ni chafu, baya, linasababisha hisia mbaya kwa msikilizaji au pia linataja mambo ya kisiri. Mifano ya kauli zinazohusisha maneno ya mwiko kutoka katika tamthilia teule ni pamoja na:

21. Katango: La, baba. Huo ni ushirikina!

Seki: Ushirikina gani? (*Kwa hasira*) Imani zetu; roho ya kuwepo kwetu; uboho wa mifupa ya jamii ndio unauita ushirikina? Wewe tangu ugomee kupashwa ...

Mama: Ahh ...Hapana; usiyalete hayo (*akiwaashiria Susa na Sota*) mbele ya watoto! Uk.19

Katika mfano wa 21, mazungumzo haya yanayotokea baada ya Katango kuja nyumbani kwao akiwa amebeba uta na mshale vitu ambavyo alikuwa ameviokota njiani. Katika jamii hii mwanamke hakuruhusiwa kubeba mata wala mshale. Babake anapomweleza kuhusu yeye kwenda kinyume na utamaduni ndipo Katango anaposema kuwa huo ni ushirikina. Ndipo babake anapoamua kuhasiri uso chanya wa Katango kwa kutumia maneno ya mwiko kuhusu Katango kugomea kupashwa tohara. Hapa babake Katango anatumia maneno ya mwiko kwa Katango ili kumuudhi na kumsababishia hisia mbaya kwake. Suala la wanawake kupashwa tohara ni mwiko katika jamii hii ndiyo sababu Mama anamwambia Seki kuwa asiyalete mbele ya wadogo zake Katango. Kwani hali hii ingemwaaibisha Katango hadharani.

2.4.4 Mzungumzaji Kutomwonea Msikilizaji Huruma

Kuna hali ambazo mzungumzaji huhitajika kumwonea msikilizaji wake huruma. Kulingana na Leech (1983) alipokuwa akishughulikia suala la upole ni kwamba kanuni ya huruma humtaka mzungumzaji kuonyesha huruma kwa msikilizaji wake hasa anapokuwa amekumbwa na janga fulani. Kwa hivyo huruma inapohitajika kuonyeshwa msikilizaji na ikosekane uso chanya wa msikilizaji huhasiriwa. Kwa mfano:

22. Katango: Unaniumiza.

Mtu I: ... Shujaa anayejitia ubabe wa kupambana na wanaume huumia? ...
Huumia kweli? (*Mtuo*) Usipokoma hata tutaku... uk.32

Katika mfano wa 22, mazungumzo haya yanayotokea baina ya watu waliotumwa na Ngwese ambaye ni mpinzani wa Katango kisiasa kuwavamia Katango na Kibwana wakiwa njiani ili kumfanya Katango abadili nia yake ya kuwania uongozi wa pango. Watu hawa waliwaumiza Katango na Kibwana. Katango anapomwambia Mtu I kwamba anamuumiza, badala ya kumwonyesha huruma pengine kwa kumwambia pole anamjibu kwa dhihaka kwa kutumia swali la balagha ambapo anamwuliza kama shujaa anayejitia ubabe wa kupamabana na wanaume huumia. Hapa Mtu I anatumia mkakati chanya wa utoupole kwa kutumia mbinu ya kutomwonea msikilizaji huruma ili kuhasiri uso chanya wa Katango.

2.4.5 Mzungumzaji Kutafuta Kutokubaliana na Msikilizaji Wake

Mbinu hii ya mkakati wa utoupole chanya inapingana na kanuni za mawasiliano ambazo zilipendekezwa na Leech (1983) alipokuwa akijishughulisha na suala la upole. Kulingana naye ni kwamba kanuni mojawapo ambayo kwayo mawasiliano huhimiliwa ni kanuni ya makubaliano. Kwa mujibu wa kanuni hii ni kwamba msemaji hutakikana akubaliane na msikilizaji wake kwa kiasi kikubwa na ikiwa hakubaliani naye basi iwe ni kwa mkakati. Zaidi ya kanuni hii kuhakikisha kuwa kuna uhusiano mwema baina ya msemaji na msikilizaji pia huepusha mawasiliano kati yao kuvunjika. Kwa upande mwingine mbinu ya kutafuta kutokubaliana na mzungumzaji kama kategoria ya mkakati chanya wa utoupole hutumiwa na msemaji ili kuvunja mawasiliano katika hali ambayo msemaji hunuia kumuudhi msikilizaji wake. Katika tamthilia ya *Pango* kuna nyakati ambazo mzungumzaji anatafuta kutokubaliana na msikilizaji wake. Kwa mfano:

23. Mama: Ngwese amewakataza watoto maji?

Seki: Uongo huo!

Katango: Si uongo! Uk.17

Katika mfano wa 23, mazungumzo haya yanatokea baada ya Susa na Sota kurudi nyumbani baada ya kukawia kwa sababu ya wingi wa watu. Wanamweleza mama yao kuhusu Ngwese kuwazuia kuteka maji katika kisima cha kawaida kwani ameizungushia seng'enge ardhi iliyokuwa na kisima akidai kuwa ilikuwa yake. Baada ya Seki kuwasili na kutaka kujua aliyewazuia watoto maji na kuambiwa ni Ngwese ndipo anaposema kuwa ulikuwa uongo. Katika muktadha huu Seki anatafuta hali ya kutokubaliana na mkewe na bintiye Katango kwa

kuwaambia kuwa walisema uongo ati Ngwese aliwakataza maji. Anasema haya kwa sababu yeye ni mfuasi hadidi wa Ngwese. Kwa hivyo Seki anatumia mkakati chanya wa utoupole hasa matumizi ya mbinu ya kutafuta kutokubaliana na wasikilizaji ili kuhasiri uso chanya wa Katango na mamake.

24. Kibwana: Mbona asifanikiwe?

Mbabekazi: Haiwezekani! *Culture, culture* bwana, unafikiri watu watakubali mwanamke awaongoze wewe? *We are not yet there!*

Kikubi: Mie nakwambia kila siku! Adui wa mwanamke ni mwanamke mwenyewe! Unasikia hayo? Unasikia? Uk. 25

Katika mfano wa 24, mazungumzo haya yanajiri katika mkahawa wa Kauleni baada ya Kibwana kusoma kwenye gazeti kuhusu nia ya Katango ya kujitoma katika ulingo wa siasa na kuwania kuwa kiongozi wa pango. Anapowaeleza wenzake ambao ni Mbabekazi na Kikubi, Mbabekazi anatafuta hali ya kutokubaliana na wenzake kwa kusema kuwa utamaduni wao haukumruhusu mwanamke kuongoza wanajamii. Katika mfano huu, Mbabekazi anatumia mbinu ya mkakati wa utoupole chanya ya msemaji kutafuta kutokubaliana na wasikilizaji wake ili kuhasiri uso chanya wa msikilizaji.

2.4.6 Mzungumzaji kumpa msikilizaji wake utambulisho usiofaa

Katika hali ya mazungumzo, msemaji huweza kumpa msikilizaji wake utambulisho usiofaa akiwa na nia ya kuvunja mawasiliano hasa katika hali ambayo mazungumzo hayamvutii. Hali kama hii ndiyo inayojitokeza katika mifano ifuatayo:

25. Katango: Uzushi wa nani?

Ngwese: Wa nani mwingine isipokuwa wewe mwanamke hapo ulipo? (*Kwa nguvu*)
Naona babako ameshindwa nawe; labda anaistahi elimu yako lakini kwangu awe na elimu au la mwanamke ni mwanamke tu! Uk. 10

Katika mfano wa 25, Ngwese anamtambulisha Katango kama mwanamke tu. Hata awe na elimu, hana tofauti yoyote na wanawake wengine anaowajua Ngwese. Katika hali hii, Ngwese

anakusudia kuuhasiri uso chanya wa Katango kwa kutumia mbinu ya mkakati chanya wa utoupole ya kumpa msikilizaji utambulisho ambao haufai.

26. Ngwese: Vitoto hivi vinavyopita kwenye ardhi ya watu ati vyataka maji.

Sakina: Kisima...? (*Ngwese anamwangalia tu*) Hamna ubaya, si ni maji tu wayatakayo? Ungewaruhusu! Uk.7

Katika mfano wa 26, Ngwese anawapatia Susa na Sota utambulisho hasi anapowaita vitoto. Haya yanatukia wakati ambapo Susa na Sota walipokuta ardhi ya kisima imezungushiwa uzio walipotaka kuteka maji. Utambulisho huu usiowafaa wasikilizaji wake unakusudia kuhasiri uso chanya wa warejelewa.

27. Mama: Katango hana neno kabisa!

Seki: Hana neno unasema? Mimi najua analo; jicho litakalogeuka chongo huanza kutokwa na chozi mapema, unasikia? Lakini mwache tu, atatambua siku moja kuwa mnyama mwenye mkia mpana hauvuki moto; maana atachomeka! (*Akimwangalia mkewe. Anajisemea*) Ama kweli wanawake wawili ni vyungu viwili vya sumu! Uk.22

Katika mfano wa 27, Seki anawapatia mkewe na Katango bintiye utambulisho usiofaa kwa kuwaita wanawake. Hata anawalinganisha na vyungu viwili vyenye sumu. Kwa maana kwamba walikuwa hatari mno. Katika hali hii Seki alikusudia kuuhasiri uso chanya wa mkewe na vilevile wa Katango kwa kuwapatia utambulisho usiofaa, kwa kuwaita wanawake.

28. Katango: Usiniguse na makono yako hayo!

Mtu I: Usiguswe kwa nini, si wewe ni mwanamke tu? Uk.32

Katika mfano wa 28, ni wazi kuwa Katango anapomkataza Mtu I kumgusa kwa ukali, Mtu I anamjibu kwa kumpa utambulisho usiofaa ili kuhasiri uso wake chanya kuwa yeye alikuwa mwanamke tu. Kwa hivyo kulingana na kauli ya Mtu I ni kwamba mwanamke ni kama chombo tu cha kumfurahisha mwanamume. Kauli yake inaonyesha anavyowadharau wanawake na vile anavyowagusagusa ili kukidhi uchu wake wa kimapenzi.

2.4.7 Mzungumzaji kumpuuza msikilizaji wake

Wakati mwingine katika mazungumzo hutokea hali ambapo msemaji humpuuza msikilizaji wake akiwa na nia ya kuyavunja mawasiliano kati yao. Hali sawa na hii ndiyo inayojitokeza katika mfano huu:

29. Ngwese: (*Anajaribu kumsogea kwa hasira*) Nitakupapata makofi wewe. Naona unanikosea adabu! Unatakiwa kuolewa utiwe adabu na mumeo.

Katango: Huu wakati mwingine! Uk. 14

Katika wa 29, Ngwese anamtisha Katango kwa kumweleza kuwa angemzaba makofi. Pia anaendelea kusema kuwa Katango anapaswa kuolewa ili atiwe adabu na mume wake. Katango kwa upande wake anaelekea kupuuza maneno haya na kumwambia Ngwese kuwa hali ilikuwa imebadilika. Kwa hivyo katika mfano huu ni kwamba Katango anatumia mbinu ya kumpuuza msikilizaji ili kuhasiri uso chanya wa Ngwese.

2.5 Mkakati ndani ya rekodi wa utoupole

Kulingana na Culpeper (1996), Mkakati huu hutumiwa katika hali ambapo msemaji anakusudia kudhuru uso wa msikilizaji wake. Msemaji hutumia kauli za dhahiri na zenye maneno machache sana lakini yenye uzito. Kauli za msemaji huwa hazina utata wowote. Mkakati huu huzingatia kanuni za ushirikiano kama zilivyopendekezwa na Grice (1975) hasa kanuni ya namna. Kanuni hii ya namna humtaka msemaji kusema maneno kwa namna iliyo wazi bila ya uvulivuli na utata wowote ili mambo yaweze kueleweka. Kwa hivyo katika mkakati ndani ya rekodi wa utoupole mzungumzaji hutoa kauli ambazo ni dhahiri na hazina utata wowote. Kauli hizi hukusudia kuhasiri uso wa msikilizaji kwa njia ya moja kwa moja. Katika mkakati huu uso hautiliwi maanani na vitendo vya kutishia uso hutendwa moja kwa moja. Kwa mfano:

30. Mbabekazi: (*Kwa sauti ya unyonge*) Ndiyo ana ujasiri sikatai lakini... (*Mtuo*) Lakini ipo haja gani ya mtu kufanya jambo ambalo unajua halifanikiwi?

Kibwana: Mbona asifanikiwe? Uk. 25

Katika mfano wa 30, mazungumzo haya ni bayana kuwa Kibwana anamuunga mkono Katango kisiasa. Kwa upande mwingine kinaya ni kwamba Mbabekazi ambaye ni wa jinsia ya kike hamuungi mkono mwanamke mwenzake. Katika kauli ya Mbabekazi, anatumia kauli ya moja

kwa moja ambayo haina utata wowote katika kufasirika. Kauli yake ina ujumbe mzito unaokusudia kuhasiri uso wa Kikubi moja kwa moja kwa kumwonyesha kuwa katika kujitolea sabili kwake kumuunga mkono Katango katika siasa ni kazi bure.

31. Mama: (*Akiwaangalia*) Ooh! Hatimaye! Lakini leo mmechelewa sana! Mligeuka miche kuota huko mlikokuwa?

Sota: Wingi wa watu! Uk.16

Katika mfano wa 31, mazungumzo haya yanayojiri baada ya Sota na Susa kurejea nyumbani kutoka kisimani baada ya muda mrefu. Mama anawaangalia na kulalamikia kuchelewa kwao kwa kutumia kauli za moja kwa moja. Katika matumizi yake ya lugha hatilii maanani suala la uso wa watoto wake. Kwa hivyo kauli zake zinakusudia kuhasiri uso wa watoto wake hasa tamanio la kutotaka kuulizwaulizwa maswali.

32. Seki: Utamaduni gani huo? Umesikia wapi wewe mwanamke ameshika mata na mishale katika jamii hii? (*Kwa nguvu zaidi*) Ehh niambie, hiyo elimu ya kizungu ndiyo inayokupa ujasiri wa kuipuuza mila?

Mama: (*kwa sauti ya chini*) Kweli Katango mwanangu!

Katango: (*Akicheka*) Mila gani baba? Kushika mata na mishale ndio kuna maana gani? Si ni mti tu na mishale (*akiangalia*) mwanzo hata upote wenyewe haupo!
Uk. 18

Katika mfano wa 32, ni bayana kuwa kauli ya baba inatumia mkakati ndani ya rekodi kwa kutumia kauli za moja kwa moja ambazo hazikusudii kuokoa uso wa msikilizaji wake. Seki anamwambia Katango kuwa utamaduni wao ulimharamisha mwanamke kushika mata na mishale. Hata anamwambia kuwa elimu ya kizungu ambayo ameipata imemkengeusha asione umuhimu wa utamaduni wake uliomlea. Naye Katango kwa upande wake anamjibu babake kwa kutumia kauli dhahiri zenye nia ya kuhasiri uso wake akimwambia kushika mata na mishale hakungemwathiri kwa njia yoyote ile. Pia anazidisha kuwa uta wenyewe ulikuwa ni mti tu na hata haukuwa na upote wake. Kwa hivyo kauli hizi za Katango zinakusudia kuhasiri uso wa babake kwa kumwonyesha kuwa baadhi ya tamaduni anazozishikilia zimepitwa na wakati na hazina maana katika jamii ya sasa.

33. Katango: Ni kweli baba, tuliviziwa na najua lazima walitumwa na Ngwese.

Seki: Ngwese! Ngwese! Ngwese! (*Kwa mama*) Usianze kushiriki kwenye mambo yasiyokuwa na msingi kama haya. Mnanipotezea wakati wangu bure. (*Kwa Katango*) Kwanza nawe kwa nini unajitia ushujaa wa kwenda kinyume na utamaduni wetu? Hujui mkia hauongozi kichwa wewe? Hujui kuchotwa kwingi huuvunja mwiko? (*Anaanza kutembea kurudi. Anawageukia Susa na Sota*). Nyie kwanza mmeacha kucheza pangoni? Uk.35

Katika mfano wa 33, mazungumzo haya yanayotokea baada ya Kibwana na Katango kuvamiwa wakiwa njiani wakitoka katika hoteli ya Kauleni na watu wanaoaminika kuwa walikuwa wametumwa na Ngwese ili kumfanya Katango kubadili nia yake. Katika mazungumzo haya Seki anatomia kauli za moja kwa moja zenye uzito kwa kusudi la kuhasiri uso wa Katango. Kwa mfano anasema kuwa hataki kupotezewa wakati. Kwake kitendo cha bintiye kuvamiwa hakimgusi mshipa. Pia anaendelea kwa kuuliza maswali ya balagha akitumia maneno ya moja kwa moja akilenga kuhasiri uso wa Katango akionyesha ambavyo Katango amekwenda kinyume na utamaduni kwa kujitia ushujaa wa kuwania kuwa kiongozi. Pia maswali yake yanakusudia kudhuru uso wa Katango kwa kumwonyesha kuwa jamii haikuwa tayari kupokea uongozi wa mwanamke.

34. Katango: (*Kwa sauti*) Msipumbazwe na matunda!

Malebo: Mkono mtupu haulambwi. Uk.47

Katika mfano wa 34, mazungumzo haya yanatokea katika uwanja ambapo hotuba za kisiasa zinatolewa na Babu anawaongoza washiriki ili kuhakikisha kuwa kila mmoja amepewa fursa yake ya kujieleza. Baada ya Katango kuhutubu akitumia mbinu ya hadithi aliwavutia watu wengi mno. Zamu ya Ngwese ilipowadia ya kuhutubu aliwahonga watu akitumia matunda. Ndipo Katango akawatahadharisha watu dhidi ya kuhadaiwa kwa kutupiwa matunda. Naye Malebo akitumia mkakati ndani ya rekodi anamwambia Katango kuwa mkono mtupu haulambwi kwamba Katango hakutoa chochote kuwapa wapiga kura ndiyo maana akashindwa vibaya sana katika uchaguzi.

35. Seki: Iweje hamkufanya lolote? (*anasogea mbele penye hadhira*) Iweje? Hamkucheza pale; najua lazima limetokea hilo. Yule hawezi kulalamika bure! Hawezi, hawezi, hawezi! Lazima pana sababu na haiwi vingine ila wao! (*Kwa sauti ya juu*) Kwa nini unanidanganya, Susa?

Susa: Baba, sikudanganyi mimi! Uk. 71

Katika mfano wa 35, mazungumzo haya yanatokea baada ya Susa na Sota kumtambua achezaye pangoni na kwenda kumweleza babu yao. Kutokana na kuhemahema kwao wanashindwa kumweleza babu yao vizuri na anafika baba yao akiwa amekasirika na kuwaamuru wamweleze babu yao waliyoyafanya pangoni lakini wanakataa. Ndipo Seki anasema maneno haya kuwa yule anaayeishi pangoni hawezi kamwe kulalamika bure. Hapo hapo anatumia mkakati ndani ya rekodi wa utoupole kwa kumwuliza Susa sababu ya kumdanganya. Swali hili linalenga kuhasiri uso wa Susa na kumfanya aonekane kuwa mtu mwongo mbele ya babu na Sota mdogo wake.

36. Ngwese: Naona unanikasirisha sasa. Nimesema mara ngapi mimi? Mali yangu sio ng'ombe wa kijiji kukamuliwa na kila mtu, unasikia?

Sakina: Ndiyo lakini ulifanya kosa kuwanyima maji. Watu huishi kwa udugu ati!

Uk.7

Katika mfano wa 36, Sakina anatumia mkakati ndani ya rekodi wa utoupole anapomwambia moja kwa moja Ngwese kuwa alifanya kosa kuwakataza watoto wa Seki kuteka maji kisimani. Katika hali hii anakusudia kuuhasiri uso wa mumewe kwani anatenda kitendo cha kutishia uso moja kwa moja.

2.6 Matumizi ya kejeli au Mkakati nje ya rekodi

Kulingana na Culpeper (1996) mkakati huu humfanya msemaji kuonekana kuwa mpole kwa msikilizaji ilhali katika hali halisi huwa hajakusudia kuonyesha upole wowote kwa msikilizaji wake. Vitendo vinavyodhuru uso hutendwa kwa kutumia implikecha. Kwa hivyo ili msikilizaji kuweza kuelewa kitendo kama chenye utoupole huhitajika kufasiri implikecha inayohusika. Ufasiri huu huhitaji uelewa wa kina wa muktadha na lengo la msemaji. Katika matumizi ya mkakati huu wa utoupole kwa kutumia kejeli msemaji huwasilisha ujumbe ulio kinyume na

aliokusudia kuwasilisha kwa msikilizaji wake. Hali kama hii ndiyo inayojitokeza katika mifano hii:

37. Ngwese: (*Akimpuuza*) Huo wivu wako! Sasa ulikuwa unafuatafuata nini huku au ulikuwa unataka kunitegea ndumba njiani? (*Kwa msisimko*) Sema kweli yako, ulikuja kunitegea ndumba ndoto yangu iweze kupombojeka sio?

(*Katango anaangua kicheko kikubwa. Anaendelea kucheka kwa muda. Kile kicheko kimkasirisha Ngwese sana*) Uk.13

Katika mfano wa 37, Ngwese anapokutana na Katango njiani anamwambia kuwa alikuwa anamfuatafuata ili kumtegea ndumba katika safari yake ya kisiasa kwa sababu ya wivu wake. Katango kwa upande wake anajibu kwa kicheko. Kicheko hiki cha Katango ni kinyume cha hisia za ndani za Katango. Katika hali hii baada ya kutupiwa cheche za matusi na Ngwese ni kinyume kwa Katango kucheka akionyesha hisia za furaha. Kwa hivyo Katango anatumia kicheko cha kejeli kuhasiri uso wa Ngwese.

38. Mama: Kwamba wamezuiwa kuchota maji na Ngwese!

Katango: Ni kweli huyo ndiye Ngwese mneyetaka kumfanya mlinzi wa Pango! Uk.17

Katika mfano wa 38, kauli ya Katango inakwenda kinyume na hisia zake kwa sababu anasema kuwa Ngwese angefanywa kiongozi baada ya kuwazuia Susa na Sota kuteka maji kisimani. Katika hali halisi ni kuwa mtu hawezi kuteuliwa kuwa kiongozi baada ya kuwakataza raia kuteka maji. Hapa Katango anatumia kejeli ili kudhuru uso wa Mama.

2.7 Kutowasilisha chochote

Kwa mujibu wa Culpeper (1996), mkakati huu wa utoupole huhusu kuwa kimya wakati ambapo upole unatarajiwa katika desturi ya jamii. Kwa mfano mtu kupokea hisani kutoka kwa mtu fulani kisha kutoshukuru au kutojibu salamu. Katika hali ya kawaida ni kwamba baada ya kupokea hisani kutoka kwa mtu fulani mtu hutarajiwa kushukuru. Kitendo cha kutoshukuru hufasiriwa kama chenye utoupole kwani huvuruga uhusiano baina ya wahusika. Vile vile kila mara mtu akiamkuliwa hutarajiwa kujibu salamu. Kutojibu salamu huvuruga utaratibu wa jamii. Pia kitendo cha mtu kuondoka bila ya kusema kwaheri hufasiriwa kama chenye utoupole. Hali

hii ya kutowasilisha chochote inajitokeza katika hali zifuatazo japo mkakati huu haujatumika sana katika tamthilia ya *Pango*:

2.7.1 Kitendo cha kutoshukuru

Katika tamaduni za jamii nyingi duniani mtu anapotendewa wema au anapopewa zawadi, mtoaji hutarajia kushukuriwa. Kitendo cha kukosa kushukuru hufasiriwa kama chenye utoupole na huvuruga mahusiano ya kijamii.

39. Kauleni: (*Kwa uchangamfu*) Siwezi kabisa kusahau mzee Ngwese. Umenisaidia pakubwa...

Ngwese: (*Kwa sauti imara*) Haya mbona basi unageuka punda? (*Kauleni kashangaa*).
Iweje kuung'ata mkono ule ule unaoujua unakulisha? Hiyo ndiyo shukrani yako? Uk.30

Katika mfano wa 39, mazungumzo haya yanatokea baina ya Kauleni na Ngwese. Hii ni baada ya Ngwese kuingia katika mkahawa wa Kauleni na kumaizi kuwa Katango alikuwa mahali pale. Kulingana na Ngwese anaona kuwa Kauleni anamsaliti kwa kushirikiana na mpinzani wake kisiasa licha ya kwamba ndiye aliyemsaidia Kauleni kupata kiwanja alikojenga hoteli yake kwa njia ya ufisadi. Kwa hivyo kulingana na Ngwese ni kwamba Kauleni hana upole kwani hakuonyesha shukrani zozote kwake. Ndipo anapomfananisha na punda kwa kitendo chake cha kukosa shukrani. Katika hali halisi za kijamii mtu anapotendewa wema na akakosa kushukuru husababisha hali inayovuruga uhusiano wa kijamii kama ile tunayoishuhudia katika madondoo haya. Kwa hivyo, Kauleni anapokosa kumshukuru Ngwese, anahasiri uso wa Ngwese na kumkasirisha.

2.7.2 Kuondoka bila ya kuaga

Mtu anapotembelea mwenzake katika jamii, inatarajiwa kwamba kipindi chake kinakapokamilika na atake kuondoka huwaaga wenyeji wake. Kitendo cha mgeni kuondoka pasi na kusema kwaheri kwa wenyeji hueleweka kama chenye utoupole. Kitendo kama hiki hupelekea kudhoofika au hata kuvunja mahusiano ya kijamii. Hili huathiri mahusiano ya kijamii kwa njia hasi. Kwa mfano:

40. Katango: Labda itafaa twende tukachunguze na hata kuwajulisha wengine. (*Kwa babu*) Babu tunarudi punde tu (*Babu anaitikia. Katango, Kikubi na Kibwana wanaondoka. Muda si muda anatokeza mama huku ameshika chano yenye makopo kadha ya uji. Anashangaa*).

Mama: Hawa nao, wamekuwa upepo kuyeyuka punde tu? Uk.59

Katika mfano wa 40, baada ya Kikubi na Kibwana kuzuru nyumbani kwa kina Katango ili kumjulua hali Katango, mama yake Katango anaondoka kwenda jikoni kuwaletea uji. Anaporejea na chano yenye makopo kadha ya uji anashangaa anapogundua kuwa Kikubi, Kibwana na Katango wameondoka bila hata ya kumuaga. Kitendo hiki cha kutowasilisha chochote kinadhuru uso wa mama na kumfanya awalinganishe na upepo unaobadili mkondo punde. Kitendo hiki huathiri mahusiano ya kijamii na kusababisha uhasama unaochangia katika kukwamiza mawasiliano na hata wakati mwingine kuvunja mawasiliano.

2.7.3 Kitendo cha kutojibu salamu

Katika hali za kawaida za kijamii, mtu anaposalimiwa hutarajiwa kujibu salamu. Kitendo cha kukosa kujibu salamu mtu anaposalimiwa hueleweka kama chenye utoupole. Hali hii hupelekea kudhoofika au kuvunjika kwa mawasiliano baina ya wahusika. Kwa mfano:

41. Kikubi: Aisee vipi?

(*Kibwana amezama tu kwenye gazeti hajibu*)

Kikubi: (*Akimwinamia*) Hello! *Mister*, gazeti linasema ulimwengu utaisha lini? Uk.24

Katika mfano wa 41, mazungumzo haya yanatokea katika mkahawa wa Kauleni ambapo Mbabekazi na Kikubi wanaingia na kumkuta Kibwana amezama katika kusoma gazeti. Kikubi anamsalimu lakini Kibwana hajibu salamu anaendelea tu kusoma gazeti. Hapa Kibwana anatomia mkakati wa utoupole wa kutowasilisha chochote kuhasiri uso wa Kibwana. Kwani katika hali ya kawaida hutarajiwa kuwa mtu anaposalimiwa ajibu salamu. Kutojibu salamu hufasiriwa kama kitendo cha utovu wa nidhamu katika jamii nyingi ulimwenguni.

2.8 HITIMISHO

Katika sura hii tumezingatia kauli za wahusika zinazodhirisha utoupole katika mazungumzo. Kauli hizi za wahusika zimeainishwa katika sehemu hii kwa kuzingatia mikakati tofauti tofauti ya utoupole kama ilivyoelezwa na Culpeper (1996). Katika sehemu hii, pia baada ya kubainisha mikakati mbalimbali ya utoupole ambayo inajitokeza katika tamthilia ya *Pango*, mikakati husika imeelezwa namna imetumika na kutolewa mifano mwafaka kutoka katika tamthilia. Kwa kufuatia maelezo na mifano ambayo imetolewa katika sura hii ni bayana kuwa wahusika katika tamthilia ya *Pango* wametumia mikakati yote mitano ya utoupole wanapoingiliana na wenzao ili kukuza msuko wa tamthilia. Vile vile, katika sura hii ni wazi kuwa wahusika wanatumia mikakati hii ya utoupole ili kudhuru uso wa wenzao katika mazungumzo. Aidha ni wazi kuwa uteuzi wa mikakati wa utoupole na mhusika unategemea uso unaotakiwa kudhuriwa.

Vile vile katika sura hii ni bayana kuwa mikakati mikuu ya utoupole hujumuisha kategoria mbalimbali. Kwa mfano mikakati chanya wa utoupole hutumia mbinu kama vile: mzungumzaji kutotaka kujihusisha na msikilizaji wake, mzungumzaji kumtusi msikilizaji wake, mzungumzaji kumpuuza msikilizaji wake, mzungumzaji kutumia maneno ya miiko katika mazungumzo, mzungumzaji kumpa msikilizaji utambulisho ambao haufai, mzungumzaji kutomwonea msikilizaji huruma na msemaji kutafuta kutokubaliana na msikilizaji wake. Nao mikakati hasi wa utoupole huhusisha mbinu kwa mfano: mzungumzaji kumrejelea msikilizaji kwa njia hasi, msemaji kuingilia faragha ya msikilizaji na msemaji kumdhalilisha msikilizaji wake. Nao mikakati ndani ya rekodi hauna vijikategoria chini yake sawa na mikakati nje ya rekodi au matumizi ya kejeli. Kwa upande wake mikakati wa utoupole wa kutowasilisha chochote una kategoria kama vile kutojibu salamu, kutoshukuru na mtu kuondoka bila ya kuwaaga wenyeji wake.

Mwisho ni kuwa wahusika katika tamthilia teule wametumia mikakati hasi ya utoupole na mikakati chanya ya utoupole kwa wingi zaidi kuliko mikakati ndani ya rekodi, matumizi ya kejeli na mikakati wa kutowasilisha chochote.

SURA YA TATU

UTOUPOLE NA UKUZAJI WA WAHUSIKA KATIKA TAMTHILIA YA PANGO

3.1 UTANGULIZI

Mtafiti katika sehemu hii anabainisha namna mikakati ya utoupole inayotumiwa na wahusika katika tamthilia ya *Pango* inachangia katika kuzikuza sifa zao. Mikakati ya utoupole ambayo imechunguzwa katika sehemu hii ni ile iliyopendekezwa na Culpeper (1996). Mikakati ya utoupole ambayo imebainishwa na kuchunguzwa katika sehemu hii ni pamoja na: Mikakati hasi ya utoupole, mikakati chanya ya utoupole, mikakati ndani ya rekodi ya utoupole na mikakati ya kutowasilisha chochote. Vile vile, mtafiti amebainisha jinsi suala zima la kidrama limebainika katika mazungumzo.

3.2 Mchango wa mikakati ya utoupole hasi katika ukuzaji wa wahusika

Kulingana na Culpeper (1996) mkakati huu hulenga kudhuru uso hasi wa msikilizaji katika mawasiliano. Mkakati huu hutumia maneno makali kwa nia ya kudhuru uso hasi wa msikilizaji ili kumwaibisha katika mazungumzo na kudhoofisha au kuvunja mawasiliano baina yao. Kupitia mkakati huu sifa za wahusika wafuatao zinakuzwa:

Ngwese anapokutana na Katango njiani anamweleza nia yake ya kuwania uongozi pia Katango anambainishia kuwa yuko katika kinyang'anyiro hicho hicho.

42. Ngwese: (*Akimwashiria mikono*) Huna chochote cha kunitisha isipokuwa huo mdomo mrefu tu na kama hujui mwenye kinywa kirefu hujichoma mwenyewe.
Nitakuwa kiongozi ... utaona tu! Utaona, nakwambia!

(*mtuo*)

Najua kinachokusumbua. Nakielewa kinachowasumbua watu kama wewe?

Katango: Unakijua ehh?

Ngwese: Ndiyo unasumbuliwa na wivu! Uk.12

Katika mfano wa 42, Ngwese anatumia mkakati hasi wa utoupole kwa kumtambulisha Katango na uhasi wa kuwa na mdomo mrefu. Ngwese anatumia mkakati huu kama njia ya kuhasiri uso hasi wa Katango kwa nia ya kuvunja mawasiliano baina yao. Kupitia mkakati huu hasi wa

utoupole sifa ya udaku ya Katango inakuzwa. Mtu mdaku ni mtu mwenye tabia ya kudadisi mambo ya watu wengine na yasiyomhusu. Kwa hivyo Katango anadokezwa na Ngwese kama mhusika mdaku na ambaye anasumbuliwa na wivu kwa ajili ya ufanisi wa wenzake.

43. Ngwese: (*Akijisemea*) Ahh, kisirani chenyewe hiki hasa! Babu alisema kukumbana na mwanamke asubuhi ni kisirani, siku nzima anaichafua. (*Kwa Katango*)
Mwanamke, unasaka nini hapa?

Katango: Je, unadhani ubabe wako unanitisha mimi? Mimi sio watoto unaowafukuza watakapo kuchota maji! Uk.10

Katika mfano wa 43, mazungumzo haya yanayotokea asubuhi moja baada ya Ngwese kukutana na Katango njiani yanadhihirisha matumizi ya mkakati hasi wa utoupole. Ngwese anatumia mkakati hasi wa utoupole hasa kwa kumhusisha Katango na uhasi wa kuwa kisirani anapokutana naye. Kupitia mkakati huu sifa ya Ngwese kuwa mwenye taasubi za kiume inakuzwa na kuenedelezwa. Kwani anawadharau sana wanawake na ndiyo sababu anapokutana na Katango asubuhi hiyo anamwona kama kisirani kwani angemvurugia siku yake nzima.

Kwa upande mwingine kupitia mkakati huu huu wa utoupole hasi, sifa ya Katango kama mhusika jasiri inakuzwa. Kwani baada ya Ngwese kumhusisha na uhasi wa kuwa kisirani anamkabili kwa kumzomea na kumwambia kuwa asije akadhani kuwa anaweza akamtisha alivyowatisha watoto alipowapata kisimani wakitaka kuteka maji.

44. Seki: Nisiyalete vipi na unamwona kigege wako huyu ananikasirisha? (*Kimya*) Wote wanadanganya; hamna maji waliyonyimwa (*Kwa Susa na Sota na kwa sauti ya juu*) Nyie mkienda kucheza michezo yenu huko na kuchelewa msije kuzua zua hapa! Hii isiwe likizo ya kusema uongo!

Mama: Seki mwenzangu hatuwezi kuwapuuza. Uk.19

Katika mfano wa 44, mazungumzo haya yanajiri baada ya Seki kuingia na kuambiwa kuwa Ngwese aliwakataza watoto kuteka maji kisimani. Seki anadai kuwa huo ulikuwa uongo na uzushi tu. Kupitia mkakati hasi wa utoupole Seki anamtambulisha Katango na uhasi wa kuwa kigege. Kupitia mkakati huu mrejelewa ambaye ni Ngwese sifa yake ya kuwa mhusika katili inakuzwa na kuenedelezwa kwani aliwakataza watoto kuteka maji kisimani. Pia sifa ya Seki kama

mhusika mpyaro inakuzwa. Mtu mpyaro ni mtu mwenye tabia ya kutumia lugha chafu katika mazungumzo. Kwani anamwita Katango kigege ambayo ni lugha chafu kumrejelea bintiye.

45. Katango: ... Najua nini? Kwani unadhani yamefichwa na yatafichwaje? (*mtuo*) Nani asiyejua kuwa alikuwa kibarakala wa wakoloni?

Ngwese: Mwanamke we! Usinitusi!

Katango: Ni ukweli na unachonyota ngozini kama upupu. (*Mtuo*) Babu yako hakushirikiana na wakoloni kuwasaliti waliopigana kuikomboa jamii yetu hii? Uk.13-14

Katika mfano wa 45, Katango anatumia mkakati hasi wa utoupole hasa kwa kutumia mbinu ya kuingilia faragha ya msikilizaji wake anaposema kuwa babake Ngwese alikuwa kibarakala wa wakoloni. Hapa sifa ya Katango ya ujasiri inakuzwa. Katango ni mwanamke jasiri anayefahamu historia ya jamii yake. Katika dondoo hili pia sifa ya babake Ngwese inakuzwa. Babake alikuwa kibarakala wa wakoloni. Kwamba alipata cheo chake baada ya kujipendekeza kwa serikali ya kibeberu. Aghalabu kiongozi wa aina hii hutumiwa na serikali za kibeberu kwa faida yao. Kwa hivyo kwa Katango kutumia mkakati hasi wa utoupole anaingilia faragha ya Ngwese na kutufichulia kuwa babake Ngwese alikuwa kiongozi mbaya kwani aliwasaliti Wanapango kwa kushirikiana na serikali za kibeberu.

46. Seki: Ushirikina gani? (*Kwa hasira*) Imani zetu; roho ya kuwepo kwetu; uboho wa mifupa ya jamii ndio unauita ushirikina? Wewe tangu ugomee kupashwa ...

Mama: Ahh... Hapana; usiyalete hayo (*akiwaashiria Susa na Sota*) mbele ya watoto!
Uk.19

Katika mfano wa 46, Seki babake Katango anatumia mkakati hasi wa utoupole hasa kwa kutumia mbinu ya msemaji kuingilia faragha ya msikilizaji wake kwa kumshutumu bintiye kuwa aligomea kupashwa tohara. Kulingana na Seki ni kuwa hii ni desturi ambayo ilistahili kutekelezwa kwa kila mwanamke katika jamii yao. Seki anamlaumu bintiye kwa kugomea desturi hii mbele ya mkewe na wanuna zake Katango. Kupitia matumizi ya mkakati huu hasi wa utoupole sifa ya Seki kuwa mhafidhina wa utamaduni inakuzwa kwani anashikilia tamaduni za jamii hata zile ambazo zimepitwa na wakati kama huu wa kuwapasha tohara wanawake.

Utamaduni wa aina hii ni hatari kwa mhusika kwani mwathiriwa anaweza kuvuja damu hadi kufa. Pia mwathiriwa hupata matatizo wakati wa kujifungua kwani njia ya uzazi hushindwa kufunguka inavyopaswa ili kukopoa mtoto. Jamii ya sasa inapaswa kupiga vita tamaduni za sampuli hii katika miktadha halisi ya kijamii.

47. Polisi II: Mzee, tumekuja kukuchukua. Unatuhumiwa kufuja mali ya umma ulipokuwa mkurugenzi katika shirika la umma!

Ngwese: (*Akitikisa kichwa*) Ahh, hapana bwana wee! (*Kwa sauti*) Nyie mnajua mnacheza na nani? Hapana, haiwezekani! (*Akimwangalia Katango*) Huu ni uzushi tu wa kulipaka matope jina langu... uk.87

Katika mfano wa 47, Polisi II anatumia mkakati hasi wa utoupole kuingilia faragha ya Ngwese. Kupitia mkakati huu sifa ya Ngwese kama mhusika fisadi inakuzwa kwani tunaelezwa kuwa Ngwese alifuja mali ya umma alipokuwa mkurugenzi katika shirika fulani la umma. Ngwese naye anapokabiliana na hali hii ya utoupole anajibainisha kuwa mhusika mwenye vitisho. Kwani anamtisha polisi II kwa kumwuliza ikiwa alijua yeye ni nani.

48. Katango: Mnataka nini?

Mtu I: (*Kwa dhihaka*) Tunakutaka wewe? Wewe mwenyewe hasa! (*Akimsogea*) Huoni raha, hivyo au tuseme hutaki kupendwa na ... (*anamshika*) kuguswa guswa... uk.32

Katika mfano wa 48, Katango anapowauliza watu wawili waliotumwa na Ngwese kuwavamia akiwa njiani na Kibwana walichokitaka, Mtu I anajibu kwa kebehi kuwa walimtaka Katango. Mtu I anatumia mkakati hasi wa utoupole kumjibu Katango. Katika mgogoro huu sifa ya watu hawa wawili ya ubabedume inajibainisha. Kwani kulingana nao mwanamke ni chombo tu cha kutoshelezea uchu wao wa kimapenzi.

49. Katango: Ndiyo maana lazima ateuliwe kiongozi afaaye!

Seki: Na huyo kiongozi afaaye ni wewe sio?

Katika mfano wa 49, Seki anatumia mkakati hasi wa utoupole hasa matumizi ya mbinu ya kutumia kebehi kwa bintiye. Katika kutumia mkakati huu Seki anajitokeza kama mhusika

mwenye ubaguzi. Kwani kwa sababu bintiye ni mwanamke na jamii yake haikuamini katika uongozi wa mwanamke basi anambagua kwa kuona kuwa hakufaa kuwaongoza wanapamgo na kuishia kutomuunga mkono katika azma yake ya kuwa kiongozi wa pango.

3.3 Mchango wa mikakati chanya ya utoupole katika ukuzaji wa wahusika

Kulingana na Culpeper (1996) mikakati chanya ya utoupole hutumiwa ili kudhuru uso chanya wa msikilizaji katika tukio la mawasiliano. Msemaji huonyesha hali ya kutoshughulikia mahitaji ya uso chanya wa msikilizaji wake. Kwa msingi huu msikilizaji hujenga mazingira ambayo yanadidimiza mahusiano mema na kuvunja mawasiliano kati yao. Kupitia mkakati huu sifa za wahusika wafuatao zimekuzwa:

50. Ngwese: Ni nini unachobwekea hapa?

Katango: Hayo nayo siyo matusi? Uk.13

Katika mfano wa 50, Ngwese anatumia mkakati chanya wa utoupole hasa matumizi ya lugha ya matusi kwa Katango kwa lengo la kuhasiri uso wake chanya. Hii ni baada ya Ngwese kumweleza Katango kuwa anasumbuliwa na wivu na ndiyo maana anajitokeza njiani asubuhi ili kumtegea ndumba katika ndoto yake kisiasa. Kisha Katango anajibu kauli yake kwa cheko na kumkasirisha Ngwese. Ndipo Ngwese anatumia lugha ya matusi kwa Katango kwa kumwuliza anachobwekea hapo. Katika matumizi ya lugha ya matusi, Ngwese anajibainisha kama mhusika mwenye matusi.

51. Mtu I: Sikiliza kirukanjia wewe! Tangu leo, ukome, unasikia? Usijitie kumpinga mzee. Kigoda cha Pango hawezi kukalia mwanamke, unasikia? Hilo halijawahi kutokea katika historia ya huku kwetu na halianzi nawe, unasikia? (*Katango anajivuta kwa maumivu*)

Katango: Unaniumiza! Uk32

Katika mfano wa 51, Mtu I anatumia mkakati chanya wa utoupole hasa matumizi ya lugha ya matusi kwa Katango. Kwani anamwita Katango kirukanjia. Kirukanjia ni mwanamke asiyependa kukaa na kutulia kwa mwanamume mmoja. Matumizi ya mkakati chanya wa utoupole na Mtu I unatubainishia bayana kuwa Mtu I ni mhusika mwenye matusi. Pia katika dondoo hili Mtu I anatumia mbinu ya kutotaka kujihusisha na msikilizaji wake ambayo ni kategoria ya mkakati

chanya wa utoupole. Anaposema kuwa kigoda cha pango hawezi kukikalia mwanamke ni dhahiri kuwa ameathiriwa na utamaduni wa jamii ambao ulitawaliwa na mfumo wa ubabedume. Kwa hivyo kauli zake zinatubainishia kuwa Mtu I pia ni mhusika mwenye ubaguzi kwani anambagua mwanamke kwa kuona kuwa hafai kuongoza pango. Vile vile sifa yake ya kuwa mhusika mwenye taasubi za kiume inajitokeza.

52. Katango: Unaniumiza.

Mtu I: (*Kwa kiburi*) Shujaa anayejitia ubabe wa kupambana na wanaume huumia? (*Akimfinya tena*) Huumia kweli? (*Mtuo*) Usipokoma hata tutaku... (*Mtu I anambana, Katango anamwuma*) Angh!! (*Anajaribu kumpiga kofi lakini Katango analikwepa. Wakati huu anatokeza Susa na Sota. Baada ya muda Sota anatoweka mbiombio*) uk.32

Katika mfano wa 52, watu waliotumwa na Ngwese kuwavamia Kibwana na Katango njiani wakitoka katika hoteli ya Kauleni, wanatumia mkakati chanya wa utoupole kwa kutoonyesha huruma kwa Katango. Hata wanamtishia kuwa asipokoma hata wangemuumiza zaidi. Kupitia mkakati huu chanya wa utoupole sifa ya ukatili wa Mtu I inabainika.

53. Mama: Ngwese amewakataza watoto maji?

Seki: Uongo huo!

Katango: Si uongo!

Katika mfano wa 53, Seki anatumia mkakati chanya wa utoupole hasa matumizi ya mbinu ya kutokubaliana na wasikilizaji wake. Kupitia mkakati huu wa utoupole, sifa ya Seki kama mhusika mbishi inawekwa bayana. Mtu mbishi ni mtu mwenye tabia ya kupinga au kutoafikiana na anayoambiwa. Hapa Seki haafikiani na madai kuwa Ngwese ambaye ni rafiki yake wa dharti aliwakataza watoto kuchota maji kisimani.

54. Kibwana: Mbona asifanikiwe?

Mbabekazi: Haiwezekani! *Culture, culture* bwana, unafikiri watu watakubali mwanamke awaongoze wewe? *We are not yet there!*

Kikubi: Mie nakwambia kila siku! Adui wa mwanamke ni mwanamke mwenyewe!

Unasikia hayo? Unasikia? Uk. 25

Katika mfano wa 54, Mbabekazi anatumia mkakati chanya wa utoupole kwa kutumia mbinu ya msemaji kutokubaliana na msikilizaji wake anaposema kuwa kulingana na utamaduni wao ni kwamba wanajamii hawangemchagua mwanamke kuwaongoza. Hata kama Mbabekazi anashawishiwa na Kikubi na Kibwana kuwa Katango alikuwa na nafasi ya kushinda, ana mtazamo tofauti kabisa. Inapokuja katika masuala ya uongozi Mbabekazi anaidunisha jinsia ya kike sana. Kupitia mkakati chanya wa utoupole anaoutumia Mbabekazi, anajibainisha kuwa yeye ni mhusika mwenye ubaguzi sana kwani anaushikilia sana mfumo wa kiubabedume kwa kuona kuwa katika jamii ya wanapango kiongozi ni sharti awe mwanamume. Kwa hivyo Mbabekazi anawabagua wanawake wenzake kwa kuona kuwa hawakufaa kuongoza pango.

55. Ngwese: Vitoto hivi vinavyopita kwenye ardhi ya watu ati vyataka maji.

Sakina: Kisima...? (*Ngwese anamwangalia tu*) Hamna ubaya, si ni maji tu wayatakayo? Ungewaruhusu! Uk.7

Katika mfano wa 55, Ngwese anatumia mkakati chanya wa utoupole kwa kuwahusisha watoto wa Seki na utambulisho usiofaa anapowaita vitoto. Hili linambainisha kama mhusika mwenye dharau kwani anawabeza watoto wa rafiki yake kwa kuwarejelea katika hali ya udogo. Sakina naye anapojibu ili kukabiliana na kitendo hiki cha utoupole anajitokeza kama mhusika mwenye uhusiano mwema kwani anamweleza Ngwese ukweli kuwa angewaruhusu watoto kuchota maji. Hapa anamhiza mumewe kuuthamini ujirani.

56. Katango: Usiniguse na makono yako hayo!

Mtu I: Usiguswe kwa nini, si wewe ni mwanamke tu? Uk.32

Katika mfano wa 56, Mtu I anatumia mkakati chanya wa utoupole apotumia utambulisho usiofaa kusema kuwa Katango ni mwanamke tu na hivyo kumgusa kwa nia ya kumtaka kimapenzi. Kwa kukabili hali hii Katango anamkataza kumgusa kwa makono yake. Katika tendo la Katango kukabili utoupole chanya wa Mtu I kumwita mwanamke tu, anajibainisha kama mhusika jasiri.

57. Ngwese: (*Anajaribu kumsogea kwa hasira*) Nitakupapata makofi wewe. Naona unanikosea adabu! Unatakiwa kuolewa utiwe adabu na mumeo.

Katango: Huu wakati mwingine! Uk. 14

Katika mfano wa 57, Ngwese anakusudia kuuhasiri uso chanya wa Katango kwa kutumia lugha ya vitisho kwamba anaweza kumpapata makofi. Mkakati huu unamtokeza Ngwese kama mhusika mwenye vitisho.

3.4 Mchango wa mkakati ndani ya rekodi wa utoupole katika kuzikuza sifa za wahusika

Kulingana na Culpeper (1996) mkakati huu wa ndani ya rekodi wa utoupole hutumiwa katika hali ambazo msemaji huwa na kusudi la kuhasiri uso wa msikilizaji wake, na hivyo basi kauli zake huwa za dhahiri na zenye maneno machache lakini yenye uzito. Katika mkakati huu uso hautiliwi maanani. Vitendo vinvyohasiri uso hutendwa moja kwa moja. Mkakati huu huzingatia kanuni za ushirikiano kama zilivyopendekezwa na Grice (1975) hasa kanuni ya namna. Kulingana na Grice kanuni ya namna humtaka msemaji kuwasilisha ujumbe kwa namna ambayo itamfanya msikilizaji kuelewa haraka. Hii ni kwa sababu ujumbe unaowasilishwa una uhusiano na mada inayojadiliwa. Mkakati huu wa kuwa ndani ya rekodi wa utoupole uanajitokeza katika hali mbalimbali na kuchangia katika kuzikuza sifa za wahusika katika tamthilia ya *Pango* ifuatavyo:

58. Seki: Utamaduni gani huo? Umesikia wapi wewe mwanamke ameshika mata na mishale katika jamii hii? (*Kwa nguvu zaidi*) Ehh niambie, hiyo elimu ya kizungu ndiyo inayokupa ujasiri wa kuipuuza mila?

Mama: (*kwa sauti ya chini*) Kweli Katango mwanangu!

Katango: (*Akicheka*) Mila gani baba? Kushika mata na mishale ndio kuna maana gani? Si ni mti tu na mishale (*akiangalia*) mwanzo hata upote wenyewe haupo!

Uk. 18

Katika mfano wa 58, Seki anatomia mkakati ndani ya rekodi wa utoupole kwa kutumia kauli za moja kwa moja ambazo lengo lake ni kuhasiri uso wa Katango. Anamwambia Katango kuwa utamaduni wao haukumruhusu mwanamke kushika uta na mishale. Pia anazidisha kuwa elimu ya

Katango ilimkengeusha na kumfanya akose kuthamini utamaduni wa jamii yake. Katika mandondoo haya sifa ya Seki kama mhusika mhafidhina wa utamaduni inajibainisha. Seki anashikilia masuala ya kitamaduni hata mengine ambayo hayana maana katika maendeleo ya jamii kama utamaduni uliomharamisha mwanamke kushika mshale na mata.

Vile vile katika muktadha huu, sifa ya Katango kama mhusika mkengeushi inajitokeza. Kutokana na elimu ya kizungu aliyoipata Katango, imemfanya kuwa mkengeushi. Mtu mkengeushi ni mtu ambaye anaishi maisha yanayopingana na utamaduni na kanuni za jamii yake. Kwa Katango utamaduni uliomkataza mwanamke kushika uta na mshale hauna maana yoyote. Vile vile katika hali ya Seki babake Katango kutumia mkakati ndani ya rekodi wa utoupole anatubainishia kuwa Katango ni mhusika msomi. Kwani anasema kuwa elimu ya kizungu ya Katango ndicho chanzo cha uasi wake wa utamaduni.

59. Katango: Ni kweli baba, tuliviziwa na najua lazima walitumwa na Ngwese.

Seki: Ngwese! Ngwese! Ngwese! (*Kwa mama*) Usianze kushiriki kwenye mambo yasiyokuwa na msingi kama haya. Mnanipotezea wakati wangu bure. (*Kwa Katango*) Kwanza nawe kwa nini unajitia ushujaa wa kwenda kinyume na uutamaduni wetu? Hujui mkia hauongozi kichwa wewe? Hujui kuchotwa kwingi huuvunja mwiko? (*Anaanza kutembea kurudi. Anawageukia Susa na Sota*). Nye kwanza mmeacha kucheza pangoni? Uk.35

Katika mfano wa 59, Seki anatumia mkakati ndani ya rekodi anaposema kuwa anapotezewa wakati baada ya kuelezwa na Katango kuwa waliviziwa na watu waliotumwa na Ngwese. Katika hali hii sifa ya Seki kama mzazi asiyejali hali ya mwanawe inajibainisha. Kwani hajali wala hamwonei imani bintiye baada ya kuvamiwa na wavamizi waliotumwa na Ngwese.

60. Katango: (*Kwa sauti*) Msipumbazwe na matunda!

Malebo: Mkono mtupu haulambwi. Uk.47

Katika mfano wa 60, Malebo anatumia mkakati ndani ya rekodi anapozungumza na Katango kuwa yeye pamoja na wafuasi wengine walivutiwa upande wa Ngwese kwa kuwa Ngwese aliwatupia matunda. Katika hali hii sifa ya mrejelewa ambaye ni Ngwese ndiyo inayokuzwa.

Ngwese anajibainisha kama mhusika fisadi kwani anawahonga wapiga kura kumchagua katika uwanja wa uchaguzi kwa kuwarushia matunda.

61. Ngwese: Naona unanikasirisha sasa. Nimesema mara ngapi mimi? Mali yangu sio ng'ombe wa kijiji kukamuliwa na kila mtu, unasikia?

Sakina: Ndiyo lakini ulifanya kosa kuwanyima maji. Watu huishi kwa udugu ati!
Uk.7

Katika mfano wa 61, kupitia mkakati ndani ya rekodi anaoutumia Sakina inabainika kuwa Ngwese ni mhusika mwenye ubinafsi kwani anasema kuwa ardhi ya kisima ilikuwa yake ndiyo maana akawakataza watoto wa Seki kuteka maji. Naye Sakina anajitokeza kama mhusika mwenye ujasiri kwani anamweleza Ngwese moja kwa moja kuwa alifanya kosa kuwakataza watoto kuchota maji kisimani bila kumwogopa.

3.5 Mchango wa matumizi ya kejeli katika kuzikuza sifa za wahusika

Culpeper (1996) anasema kuwa mkakati huu wa utoupole humfanya msemaji kuonekana kuwa mpole lakini katika hali halisi huwa hajakusudia kuonyesha upole wowote kwa msikilizaji wake. Msemaji hufanya juhudi za kuonyesha upole kwa msikilizaji wake lakini katika hali halisi huwa hajakusudia kuwa mpole kwa msikilizaji wake. Huwasilisha vitendo vinavyohasiri uso kwa kutumia implikecha ambapo msikilizaji huachwa afasiri alilokusudia msemaji kuwasilisha. Hata hivyo ufasiri wa msikilizaji hudhibitiwa na muktadha wa mazungumzo. Mkakati huu pia unapotumiwa na wahusika huchangia katika ukuzaji wa sifa zao kwa mfano:

62. Mama: Kwamba wamezuiwa kuchota maji na Ngwese!

Katango: Ni kweli huyo ndiye Ngwese mnayetaka kumfanya mlinzi wa Pango! Uk.17

Katika mfano wa 62, mazungumzo haya yanatokea baada ya mama kubaini kuwa Ngwese aliwakataza watoto wake kuchota maji kisimani. Mama anashangazwa na hili. Katango anatumia mkakati wa utoupole wa kutumia kejeli anapomwambia mamake kuwa baada ya Ngwese kuwakataza nduguze kuchota maji kisimani ndiye kiongozi anayefaa kuchaguliwa. Anatumia mkakati huu wa matumizi ya kejeli ili kuzua ucheshi. Hivyo basi Katango anajibainisha kama mhusika mcheshi.

3.6 Mchango wa kutowasilisha chochote katika kuzikuza sifa za wahusika

Kulingana na Culpeper (1996) anasema kuwa mkakati wa kutowasilisha chochote huhusu kuwa kimya wakati ambapo upole unatarajiwa katika desturi ya jamii. Mkakati huu huweza kujitokeza katika hali ambapo mtu anapokea hisani kutoka kwa mwenzake kisha anakosa kushukuru au mtu anaposalimiwa na akakosa kujibu salamu hizo. Kidesturi ni kwamba baada ya kupokea hisani mtu hubidiika kushukuru na pia mtu anapoamkuliwa hutarajiwa wajibu salamu. Hivyo basi kitendo cha mtu kukosa kujibu salamu au kukosa kushukuru hufasiriwa kama chenye utoupole katika jamii. Vile vile kitendo cha mgeni kuondoka bila ya kuwaaga wenyeji huweza pia kufasiriwa kama chenye utoupole. Matendo haya yote huvuruga utaratibu wa kijamii na kusababisha uhasama miongoni mwa wahusika. Uhasama huu hudhoofisha au huvunja mawasiliano baina ya wahusika. Hali kama hii ndiyo inayodhihirika katika mazungumzo yafuatayo:

63. Kauleni: (*Kwa uchangamfu*) Siwezi kabisa kusahau mzee Ngwese. Umenisaidia pakubwa...

Ngwese: (*Kwa sauti imara*) Haya mbona basi unageuka punda? (*Kauleni kashangaa*).
Iweje kuung'ata mkono ule ule unaojua unakulisha? Hiyo ndiyo shukrani yako? Uk.30

Katika mfano wa 63, Kauleni ambaye ni mmiliki wa hoteli alisaidiwa na Ngwese kupata uwanja alikojenga hoteli yake. Licha ya kusaidiwa huku na Ngwese Kauleni huonyeshi shukrani zozote kwa mfadhili wake. Hata anashirikiana na Katango ambaye ni mpinzani wa Ngwese kisiasa. Katika dayalojia hii sifa ya Kauleni ya usaliti inajibainisha wazi.

64. Katango: Labda itafaa twende tukachunguze na hata kuwajulisha wengine. (*Kwa babu*) Babu tunarudi punde tu (*Babu anaitikia. Katango, Kikubi na Kibwana wanaondoka. Muda si muda anatokeza mama huku ameshika chano yenye makopo kadha ya uji. Anashangaa*).

Mama: Hawa nao, wamekuwa upepo kuyeyuka punde tu? Uk.59

Katika mfano wa 64, Kikubi na Kibwana wanamtembelea Katango nyumbani kwao ili kujua anavyoendelea baada ya ushinde wake. Halafu wanaondoka pamoja na Katango bila ya kumuaga

mama Katango. Hata Mama anapokuja na makopo kadha ya uji anashangaa anapogundua kuwa walikuwa washaondoka bila ya kumwambia kwaheri. Kupitia mkakati huu wa kutowasilisha chochote unaotumiwa na kina Kikubi na Kibwana sifa ya Mama kama mhusika karimu inakuzwa.

3.7 Hitimisho

Katika sura hii, utafiti huu umejikita katika kuzijadili sifa za wahusika katika tamthilia ya *Pango* kama zinavyobainika kupitia mikakati mbalimbali ya utoupole ambayo wanaitumia katika maingiliano yao mbalimbali. Sifa za wahusika mbalimbali zimeelezwa kama zinavyojitokeza kupitia matumizi yao ya lugha. Fauka ya hayo, imebainika kuwa mwingiliano wa wahusika hawa umetawaliwa na migogoro mbalimbali ambayo inawafanya kutumia mikakati mbalimbali ya utoupole ili kuvunja mahusiano miongoni mwao.

SURA YA NNE

MIKAKATI YA UTOUPOLE NA UKUZAJI WA MAUDHUI

4.1 UTANGULIZI

Sura hii inaangazia namna maudhui yanakuzwa kupitia mikakati mbalimbali ya utoupole. Mtafiti amechunguza jinsi mikakati ya utoupole iliyopendekezwa na Culpeper (1996) inakuza maudhui. Mikakati ya utoupole ambayo imebainishwa na kuchunguzwa katika sehemu hii ni pamoja na: Mkakati hasi wa utoupole, mkakati chanya wa utoupole, mkakati ndani ya rekodi wa utoupole, matumizi ya kejeli na kutowasilisha chochote. Maudhui yanayokuzwa na kuendelezwa kupitia mikakati hii ya utoupole ni pamoja na: utamaduni, ukatili, ukoloni mamboleo, ndoa, taasubi za kiume, ushirikina, ufisadi na usaliti.

4.2 Mchango wa mkakati hasi wa utoupole katika kukuza maudhui

Kulingana na Culpeper (1996), mkakati huu hukusudiwa kudhuru uso hasi wa msikilizaji. Katika mkakati huu mzungumzaji huzidisha makali na hali zinazotishia uso wa msikilizaji wake. Katika mkakati huu msemaji huwa na ufahamu kuwa kauli zake huenda zikamkasirisha msikilizaji wake au hata zikazua aibu. Kupitia makakati huu mzungumzaji hupita mipaka na kuingilia uhuru wa msikilizaji wake. Mkakati huu umetumika katika tamthilia ya Pango kukuza na kuendeleza maudhui yafuatayo:

65. Seki: Ushirikina gani? (*Kwa hasira*) Imani zetu; roho ya kuwepo kwetu; uboho wa mifupa ya jamii ndio unauita ushirikina? Wewe tangu ugomee kupashwa ...

Mama: Ahh... Hapana; usiyalete hayo (*akiwaashiria Susa na Sota*) mbele ya watoto!

Uk.19

Katika mfano wa 65, Seki anatumia mkakati hasi wa utoupole hasa matumizi ya mbinu ya kuingilia faragha ya msikilizaji kuendeleza maudhui ya utamaduni. Utamaduni unaojitokeza katika dondoo hili ni ule unaomkandamiza mwanamke. Seki babake Katango anamlaumu bintiye kwa kukataa kupashwa tohara. Katika jamii hii, desturi hii ilitahili kutekelezwa kwa kila mwanamke. Seki anamshutumumu bintiye kwa kugomea desturi hii hadharani mbele ya mkewe na nduguze. Mama anamtahadharisha mumewe dhidi ya kuzungumzia masuala ya utamaduni mbele ya watoto kwani kulingana naye masuala ya tohara yafaa yawe ya faraghani.

66. Katango: ... Najua nini? Kwani unadhani yamefichwa na yatafichwaje? (*mtuo*) Nani asiyejua kuwa alikuwa kibarakala wa wakoloni?

Ngwese: Mwanamke we! Usinitusi!

Katango: Ni ukweli na unachonyota ngozini kama upupu. (Mtu) Babu yako hakushirikiana na wakoloni kuwasaliti waliopigana kuikomboa jamii yetu hii? Uk.12

Katika mfano wa 66, Katango anatumia mkakati hasi wa utoupole kuhasiri uso hasi wa Ngwese hasa kwa kuingilia faragha ya Ngwese anapomwambia kuwa babake alikuwa kibarakala wa wakoloni. Hapa maudhui ya usaliti yanaendelezwa kwani babake Ngwese aliwasaliti Wanapango wenzake kwa kushirikiana na wakoloni hali ambayo ilitatiza kupatikana kwa ukombozi.

67. Polisi II: Mzee, tumekuja kukuchukua. Unatuhumiwa kufuja mali ya umma ulipokuwa mkurugenzi katika shirika la umma!

Ngwese: (*Akitikisa kichwa*) Ahh, hapana bwana wee! (Kwa sauti) Nyie mnajua mnacheza na nani? Hapana, haiwezekani! (Akimwangalia Katango) Huu ni uzushi tu wa kulipaka matope jina langu... uk.87

Katika mfano wa 67, kupitia mkakati hasi wa utoupole ambao unatumiwa na Polisi II, hasa kwa kuingilia faragha ya Ngwese anapomwambia kuwa, anatuhumiwa kwa kufuja mali ya umma alipokuwa mkurugenzi katika shirika fulani la umma. Hapa maudhui ya ufidadi yanakuzwa na kuendelezwa. Ufidadi ni matumizi mabaya ya mali ya umma. Ni bayana kuwa Ngwese alitumia mali ya umma kujifaidi wakati ambapo alikuwa mkurugenzi wa shirika la umma ndiposa alitakiwa ajibu mashtaka yaliyohusiana na ufujaji huo wa mali ya umma.

68. Ngwese: (*Akijisemea*) Ahh, kisirani chenyewe hiki hasa! Babu alisema kukumbana na mwanamke asubuhi ni kisirani, siku nzima anaichafua. (*Kwa Katango*) Mwanamke, unasaka nini hapa?

Katango: Je, unadhani ubabe wako unanitisha mimi? Mimi sio watoto unaowafukuza watakapo kuchota maji! Uk.10

Katika mfano wa 68, Ngwese anatumia mkakati hasi wa utoupole hasa kwa kumhusisha Katango na uhasi wa kuwa kisirani anapokutana naye njiani asubuhi. Katika dayalojia hii maudhui ya taasubi za kiume yanaendelezwa. Kwa sababu ya taasubi za kiume, Ngwese anamdunisha Katango kwa kumwona kama mtu mwenye nuhusi ya kumchafulia siku yake nzima anapokutana naye njiani asubuhi.

69. Ngwese: ... Huna chochote cha kunitisha isipokuwa huo mdomo mrefu tu na

kama hujui mwenye kinywa kirefu hujichoma mwenyewe.

Nitakuwa

kiongozi ... utaona tu! Utaona, nakwambia!

(mtuo)

Najua kinachokusumbua. Nakielewa kinachowasumbua watu kama wewe?

Katango: Unakijua ehh?

Ngwese: Ndiyo unasumbuliwa na wivu! Uk.12

Aidha katika mfano wa 69, Ngwese anatumia mkakati hasi wa utoupole kuhasiri uso hasi wa Katango na kuendeleza pia maudhui ya taasubi za kiume. Anasema kuwa kamwe mwanamke hawezi kumtisha kwa sababu jamii hii inatawaliwa na mfumo wa ubabedume.

4.3 Mchango wa mkakati chanya wa utoupole katika kukuza maudhui

Kwa mujibu wa Culpeper (1996), mkakati huu hukusudiwa kudhuru uso chanya wa msikilizaji hasa matamano ya msikilizaji ya kutaka kukubaliwa kama sehemu ya kundi katika jamii. Mkakati huu umetumiwa kuendeleza maudhui ifuatavyo:

70. Sakina: Ni kosa ndiyo.

Ngwese: *(Akiashiria)* Kwanza wewe, rudi huko ulikokuwa! Unanitilia ukuba siku yangu wewe. Uk.7

Katika mfano wa 70, Ngwese anatumia mkakati huu chanya wa utoupole hasa kwa kutotaka kujihusisha na mkewe anapomwamuru kurudi alikokuwa. Katika hali hii anaendeleza maudhui ya taasubi za kiume kwani kulingana naye ni kwamba kujibizana na mwanamke ni kujiletea nuksi.

Vile vile maudhui haya ya taasubi za kiume yanaendelezwa na Ngwese, anapokutana njiani na Katango na baada ya kujibizana naye, anamwuliza akitumia mkakati chanya wa utoupole kwa kutumia lugha ya matusi alichokuwa akibwekea. Katika hali hii ni bayana kuwa Ngwese aliwadunisha wanawake wote.

71. Kibwana: Mbona asifanikiwe?

Mbabekazi: Haiwezekani! *Culture, culture* bwana, unafikiri watu watakubali mwanamke awaongoze wewe? *We are not yet there!*

Kikubi: Mie nakwambia kila siku! Adui wa mwanamke ni mwanamke mwenyewe! Unasikia hayo? Unasikia? Uk. 25

Katika mfano wa 71, Mbabekzai anatumia mkakati chanya wa utoupole hasa kwa kutafuta hali ya kutokubaliana na wenzake kwa sababu katika jamii yao utamaduni haukuuruhusu mwanamke kutawala. Katika hali hii Mbabekazi amesongwa na utamaduni wa jadi unaogawa majukumu kwa misingi ya kijinsia. Kulingana naye haamini kuwa wanapango wangeweza kumchagua Katango kama kiongozi wao. Mbabekazi anaona kwamba Katango hangeweza kuongoza Pango kwa vile yeye ni mwanamke. Zaidi ya kuonyeshwa na Kikubi na Kibwana kuwa Katango ana nafasi ya kushinda katika kinyang'anyiro, Mbabekazi ana mtazamo tofauti kabisa kwa sababu amefumbwa macho na utamaduni wa jamii ambao unadunisha jinsia ya kike katika suala la uongozi.

Wafula na Njogu (2007) wanasema kwamba wanaotetea ufeministi wa kiafrika wanaamini kuwa udunishwaji wa mwanamke unatokana na mila na itikadi za Kiafrika. Kulingana na mila na itikadi hizi ni kwamba wanaume hupewa majukumu tofauti na wanawake. Majukumu haya humpendelea mwanamume kuliko mwanamke. Kwa hivyo, ni tamaduni hizi kandamizi amabzo zimemwathiri Mbabekazi na kumfanya kuona jinsia ya kike kama ambayo haiwezi kuongoza jamii.

72. Ngwese: (*Anajaribu kumsogea kwa hasira*) Nitakupapata makofi wewe. Naona unanikosea adabu! Unatakiwa kuolewa utiwe adabu na mumeo.

Katango: Huu wakati mwingine! Uk. 14

Katika mfano wa 72, Ngwese anatumia mkakati chanya wa utoupole hasa matumizi ya vitisho ili kuhasiri uso chanya wa Katango. Katika dondoo hili maudhui ya ndoa yanaendelezwa kwani Ngwese anamhiza Katango kumtafuta mwanamume akamuoe. Katika dayalojia hii ni wazi kuwa asasi ya ndoa inampa mwanamume mamlaka ya kumwadhibu mke wake. Kwa vile jambo hili ni halali katika jamii, mwanamke hawezi kupinga wala kujitetea kwa kuwasilisha malalamishi yake mahali popote.

73. Katango: Uzushi wa nani?

Ngwese: Wa nani mwingine isipokuwa wewe mwanamke hapo ulipo? (*Kwa nguvu*)

Naona babako ameshindwa nawe; labda anaistahi elimu yako lakini kwangu awe na elimu au la mwanamke ni mwanamke tu! Uk. 10

Katika mfano wa 73, Ngwese anatumia mkakati chanya wa utoupole kuendeleza maudhui ya elimu. Kwani kulingana naye ni kuwa mwanamke ni mwanamke tu awe na elimu au la. Anasema hivi kwa sababu anaona kwamba Katango anajitia ujasiri wa kumpinga kisiasa kwa sababu amesoma. Katika mazungumzo haya, Ngwese anaonekana kuamini ya kwamba mwanamke hapaswi kuwa na elimu kama mwanamume. Hata hivyo Katango anaonekana kukiuka mtazamo huu wa kitamaduni anapojipatia elimu na kuhitimu kuwa mwalimu.

74. Mtu I: Sikiliza kirukanjia wewe! Tangu leo, ukome, unasikia? Usijitie kumpinga

mzee. Kigoda cha Pango hawezi kukalia mwanamke, unasikia? Hilo

halijawahi kutokea katika historia ya huku kwetu na halianzi

nawe, unasikia? (*Katango anajivuta kwa maumivu*)

Katango: Unaniumiza! Uk32

Katika mfano wa 74, Mtu I anatumia mkakati chanya wa utoupole kuendeleza maudhui ya ukatili. Hawa watu walitumwa na Ngwese kumvamia Katango na Kibwana wakiwa njiani ili kumtia Katango woga na kumfanya aghairi nia yake kisiasa. Katika majibizano kati yao

inabainika kuwa watu hawa walimuumba Katango. Hii ni dhahirisho kuwa katika jamii hii mfumo wa ubabedume ulimpa mwanamke nafasi ya pili baada ya mwanamume. Kwa hivyo hakupaswa kuongoza jamii.

Pia maudhui haya ya ukatili yanaendelezwa katika mazungumzo haya:

75. Mama: Ngwese amewakataza watoto maji?

Seki: Uongo huo!

Katango: Si uongo! Uk.17

Katika mfano wa 75, Mama anatumia mkakati chanya wa utoupole kuendeleza maudhui ya ukatili ambao unaendelezwa na Ngwese dhidi ya familia yake. Kwani Ngwese aliwakataza watoto wake kuchota maji kisimani. Malalamishi ya Mama yanapingwa na Seki kwa sababu Seki anamuunga Ngwese mkono kisiasa na hataki kulipaka jina lake tope la aina yoyote.

4.4 Mchango wa mkakati ndani ya rekodi wa utoupole katika ukuzaji wa maudhui

Kulingana na Culpeper (1996), mkakati huu hutumiwa katika hali ambapo msemaji anakusudia kudhuru uso wa msikilizaji wake. Msemaji hutumia kauli za dhahiri na zenye maneno machache sana lakini yenye uzito. Kauli za msemaji huwa hazina utata wowote. Mkakati huu huzingatia kanuni za ushirikiano kama zilivyopendekezwa na Grice (1975) hasa kanuni ya namna. Kanuni hii ya namna humtaka msemaji kusema maneno kwa namna iliyo wazi bila ya uvulivuli na utata wowote ili mambo yaweze kueleweka. Kwa hivyo katika mkakati ndani ya rekodi wa utoupole mzungumzaji hutoa kauli ambazo ni dhahiri na hazina utata wowote. Kauli hizi hukusudia kuhasiri uso wa msikilizaji kwa njia ya moja kwa moja. Katika mkakati huu uso hautiliwi maanani na vitendo vya kutishia uso hutendwa moja kwa moja. Mkakati huu unatumika kukuza maudhui katika tamthilia teule ifuatavyo:

76. Seki: Utamaduni gani huo? Umesikia wapi wewe mwanamke ameshika mata na mishale katika jamii hii? (*Kwa nguvu zaidi*) Ehh niambie, hiyo elimu ya kizungu ndiyo inayokupa ujasiri wa kuipuuza mila?

Mama: (*kwa sauti ya chini*) Kweli Katango mwanangu!

Katango: (*Akicheka*) Mila gani baba? Kushika mata na mishale ndio kuna maana gani?

Si ni mti tu na mishale (*akiangalia*) mwanzo hata upote wenyewe haupo!

Uk. 18

Katika mfano wa 76, Seki anatumia mkakati ndani ya rekodi kuendeleza maudhui ya utamaduni. Kutokana na athari za tamaduni kandamizi za jamii yake dhidi ya mwanamke, anamkaripia Katango kuwa ameshika uta na mishale mikononi. Kulingana naye ni kuwa ni wanaume tu walioruhusiwa kushika ala hizi. Kwa mtazamo wa Seki ni kwamba ile elimu ya kizungu aliyoipata Katango ndiyo iliyompa ujasiri wa kupuuza desturi za jamii yake. Hata hivyo tukitazama kwa jicho pevu ni kwamba jamii hii ya Pango inatawaliwa na ubabedume na inasingizia elimu ya kizungu kuwa pingamizi ya mila kandamizi.

Watetezi wa ufeministi wa Kiafrika wanasema kuwa mwanamke wa kiafrika anaweza kujikomboa kwa kutumia njia mbalimbali na kuishi bila unyanyasaji huu. Elimu inapendekezwa kuwa njia mojawapo ambayo inaweza kutumika kumkomboa mwanamke. Mhusika Katango amepata elimu na hivyo basi mtazamo wake wa ulimwengu ni sambamba na ule wa wafeministi wa Kiafrika.

77. Mbabekazi: (*Kwa sauti ya unyonge*) Ndiyo ana ujasiri sikatai lakini... (*Mtuo*) Lakini ipo haja gani ya mtu kufanya jambo ambalo unajua halifanikiwi?

Kibwana: Mbona asifanikiwe? Uk. 25

Katika mfano wa 77, Mbabekazi anatumia mkakati ndani ya rekodi kuendeleza maudhui ya Ubaguzi. Kulingana naye ni kuwa haina haja ya Katango kujitia ujasiri kuwania uongozi ilhali anaelewa fika kuwa hangefaulu. Kwani utamaduni wa Wanapango haungeruhusu mwanamke kuwaongoza. Kwa hivyo Mbabekazi anamwona Katango kama mtu ambaye hafai kuwania uongozi wa Pango. Kwa hivyo yeye anapendelea uongozi wa wanaume.

Pia maudhui haya ya ubaguzi yanaendelezwa na Seki anapotumia mkakati ndani ya rekodi kama inavyodhihirika katika dondoo hili:

78. Katango: Ni kweli baba, tuliviziwa na najua lazima walitumwa na Ngwese.

Seki: Ngwese! Ngwese! Ngwese! (*Kwa mama*) Usianze kushiriki kwenye mambo yasiyokuwa na msingi kama haya. Mnanipotezea wakati wangu bure. (*Kwa Katango*) Kwanza nawe kwa nini unajitia ushujaa wa kwenda kinyume na uatamaduni wetu? Hujui mkia hauongozi kichwa wewe? Hujui kuchotwa kwingi huuvunja mwiko? (*Anaanza kutembea kurudi. Anawageukia Susa na Sota*). Nyie kwanza mmeacha kucheza pangoni? Uk.35

Katika mfano wa 78, Seki kwa upande wake anamwona Katango kama mtu asiyefaa kuwaongoza wanapango. Hivyo basi yeye anampendelea rafiki yake Ngwese. Hata anajaribu kumshawishi Katango asiwanye uongozi wa Pango. Hata hivyo Katango kwa upande wake anaelekea kutoachilia mbali azimio lake na hata kudai kuwa ana haki kama mwanapango mwingine kuwania uongozi.

79. Katango: (Kwa sauti) Msipumbazwe na matunda!

Malebo: Mkono mtupu haulambwi. Uk.47

Katika mfano wa 79, Katango anatumia mkakati ndani ya rekodi kuendeleza maudhui ya ufasidi unaotekezwa na Ngwese. Anawaonya wapiga kura dhidi ya kudanganywa kwa matunda. Hii ni baada ya Ngwese kuwahonga wapiga kura kwa kuwarushia matunda na kuishia kuwavutia upande wake na kupata ushindi.

4.5 Mchango wa matumizi ya kejeli katika kukuza maudhui

Culpeper (1996) anasema kuwa mkakati huu wa utoupole humfanya msemaji kuonekana kuwa mpole lakini katika hali halisi huwa hajakusudia kuonyesha upole wowote kwa msikilizaji wake. Msemaji hufanya juhudi za kuonyesha upole kwa msikilizaji wake lakini katika hali halisi huwa hajakusudia kuwa mpole kwa msikilizaji wake. Huwasilisha vitendo vinavyohasiri uso kwa kutumia implikecha ambapo msikilizaji huachwa afasiri alilokusudia msemaji kuwasilisha. Hata hivyo ufasiri wa msikilizaji hudhibitiwa na muktadha wa mazungumzo. Mkakati huu pia unapotumiwa na wahusika huchangia katika ukuzaji wa maudhui kwa mfano:

80. Mama: Kwamba wamezuiwa kuchota maji na Ngwese!

Katango: Ni kweli huyo ndiye Ngwese mnayetaka kumfanya mlinzi wa Pango! Uk. 7

Katika mfano wa 80, Kauli ya Katango inakwenda kinyume na hisia zake kwa sababu anasema kuwa Ngwese angefanywa kiongozi baada ya kuwakataza wanuna wake kuteka maji kisimani. Katika hali ya kawaida ni kwamba mtu hawezi kufanywa kiongozi kwa kuwazuia wengine kutumia rasilmali za nchi. Kwa hivyo, kupitia mkakati huu wa matumizi ya kejeli wa Katango maudhui ya ubinafsi yanaendelezwa, kwani Ngwese anawazuia wengine kuteka maji ili yeye ayatumie pekee yake.

4.6 Mchango wa mkakati wa Kutowasilisha chochote katika kukuza maudhui

Culpeper (1996) anasema kuwa mkakati huu wa utoupole huhusu kuwa kimya wakati ambapo upole unatarajiwa katika desturi ya jamii. Kwa mfano mtu kupokea hisani kutoka kwa mtu fulani kisha kutoshukuru au kutojibu salamu. Katika hali ya kawaida ni kwamba baada ya kupokea hisani kutoka kwa mtu fulani mtu hutarajiwa kushukuru. Kitendo cha kutoshukuru hufasiriwa kama chenye utoupole kwani huvuruga uhusiano baina ya wahusika. Vile vile kila mara mtu akiamkuliwa hutarajiwa kujibu salamu. Kutojibu salamu huvuruga utaratibu wa jamii. Pia kitendo cha mtu kuondoka bila ya kusema kwaheri hufasiriwa kama chenye utoupole. Kwa mfano. Hali hii ya kutowasilisha chochote unakuza maudhui ifuatavyo:

81. Kauleni: (*Kwa uchangamfu*) Siwezi kabisa kusahau mzee Ngwese. Umenisaidia pakubwa...

Ngwese: (*Kwa sauti imara*) Haya mbona basi unageuka punda? (*Kauleni kashangaa*). Iweje kuung'ata mkono ule ule unaoujua unakulisha? Hiyo ndiyo shukrani yako? Uk.30

Katika mfano wa 81, Kauleni anatumia mkakati wa kutowasilisha chochote kuendeleza maudhui ya usaliti. Kwani alisaidiwa na Ngwese kupata kiwanja alikojenga mkahawa wake, halafu anashirikiana na Katango mpinzani wa Ngwese kisiasa. Kwa hivyo kulingana na Ngwese, Kauleni ni mhusika asiye na shukrani.

82. Katango: Labda itafaa twende tukachunguze na hata kuwajulisha wengine. (*Kwa babu*) Babu tunarudi punde tu (*Babu anaitikia. Katango, Kikubi na Kibwana wanaondoka. Muda si muda anatokeza mama huku ameshika chano yenye makopo kadha ya uji. Anashangaa*).

Mama: Hawa nao, wamekuwa upepo kuyeyuka punde tu? Uk.59

Katika mfano wa 82, Kikubi na Kibwana wanatumia mkakati wa kutowasilisha chochote wanapoenda kumtembelea Katango ili kujua anavyoendelea baada ya ushinde. Kisha wanaondoka pamoja na Katango bila ya kumuaga mama Katango. Mama anapokuja na makopo kadha ya uji anashangaa kugundua kuwa washaondoka bila ya kumuaga. Kupitia tendo hili maudhui ya ukarimu yanakuzwa.

4.7 Hitimisho

Katika sura hii tulinuia kudhihirisha mikakati ya utoupole inavyodhihirika ili kukuza maudhui. Mwandishi kupitia wahusika mbalimbali amedhihirisha mikakati mbalimbali ya utoupole ambayo imemwezesha kukuza maudhui mbalimbali katika tamthilia ya *Pango*.

SURA YA TANO

HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

5.1 Utangulizi

Sehemu hii, inatoa muhtasari wa tasnifu nzima na kufafanua ikiwa madhumuni ya utafiti huu yameafikiwa au la. Hii ni baada ya kuhitimisha uchunguzi na kuchanganua data katika sura ya tatu na nne. Aidha, sura hii inaangazia changamoto ambazo tulikabiliana nazo katika uchunguzi huu na hatimaye kutoa mapendekezo kuhusu tafiti zijazo ambazo zinastahili kufanywa kuhusu suala la utoupole katika mawasiliano.

5.2 Kutathmini Ufanisi wa Madhumuni ya Utafiti

Utafiti huu ulidhamiria kubainisha mikakati ya utoupole ambayo inatumiwa na wahusika wanapoingiliana na wenzao ili kufanikisha mazungumzo yao. Pia, mtafiti alikusudia kubainisha namna mikakati ya utoupole inayotumiwa na wahusika katika tamthilia ya *Pango* inachangia katika ukuzaji wa sifa zao. Vilevile, mtafiti alilenga kubainisha namna mikakati ya utoupole inayotumiwa na wahusika inaendeleza maudhui katika tamthilia ya *Pango*.

Madhumuni ya kwanza ambayo ni kubainisha mikakati ya utoupole ambayo inatumiwa na wahusika wanapoingiliana na wenzao ili kufanikisha mazungumzo yao yameafikiwa. Jinsi utafiti huu unavyodhihirisha katika sura ya pili, wahusika mbalimbali wanaitumia mikakati yote mitano ya utoupole katika maingiliano yao na wahusika wengine ili kupujua uso. Hii mikakati ni pamoja na: Mkakati hasi wa utoupole, mkakati chanya wa utoupole, mkakati ndani ya rekodi wa utoupole, matumizi ya kejeli na kutowasilisha chochote. Matumizi ya mkakati hasi wa utoupole pamoja na kategoria zake yanabainika kupitia njia mbalimbali kwa mfano:

Ngwese anaupujua uso hasi wa Katango kwa kumhusisha na uhasi anapomwita kisirani. Katika mfano wa 7. Katika hali hii Ngwese anatumia mkakati hasi wa utoupole hasa kwa kutumia mbinu ya kumrejelea msikilizaji kwa njia hasi ili kuvunja mawasiliano yoyote kati yao. Hii ni baada ya Ngwese kukutana na Katango njiani asubuhi. Kwa ujasiri Katango anajikinga dhidi ya upujufu huu kwa kumkabili Ngwese kwa kumwambia kuwa asidhani yeye ni kama wadogo wake ambao Ngwese aliwazuia kuteka maji kisimani. Pia, katika mfano wa 11, Polisi anatumia mbinu ya mzungumzaji kuingilia faragha ya msikilizaji ili kuupujua uso hasi wa Ngwese.

Anamwambia Ngwese kuwa walitumwa na mamlaka ya juu kuja kumchukua kwani alipokuwa mkurugenzi katika shirika la umma alifuja mali ya umma. Ngwese anakabili suala hili la utoupole kwa kutenda kitendo kinachodhuru uso anapotumia vitisho kwa polisi, anapomwuliza kama walijua yeye alikuwa nani.

Kwa upande mwingine mkakati chanya wa utoupole umetumiwa na wahusika mbalimbali ili kuhasiri uso chanya wa wahusika wengine. Kwa mfano, katika mfano wa 19, Ngwese anamwuliza Katango anachobwekea. Ngwese katika hali hii anatumia mbinu ya matumizi ya lugha ya matusi ili kukatiza mawasiliano kati yake na Katango ambaye ni mpinzani wake kisiasa. Vilevile, katika mfano wa 21, Seki ambaye ni babake Katango anaudhuru uso chanya wa Katango kwa kutumia lugha ya miiko anapomwambia Katango mbele ya mamake na wanuna zake kuwa alikuwa amegoma kupashwa tohara. Pia, katika mfano wa 24, Mbabekazi anatafuta hali ya kutokubaliana na wenzake kwa lengo la kupujua uso wao anapowaambia kwamba utamaduni wao haungemruhusu mwanamke kuongoza jamii. Naye Kikubi anakabili suala hili la utoupole kwa kutenda kitendo kinachodhuru uso kwa kumwambia Mbabekazi kuwa adui wa mwanamke ni mwanamke.

Pia wahusika katika tamthilia hii ya *Pango* wametumia mkakati ndani ya rekodi. Mathalan, katika mfano wa 31, Seki anamwambia Katango kuwa elimu ya kizungu ambayo Katango aliipata ilimkengeusha hadi akakosa kuona umuhimu wa utamaduni uliomzaa na kumlea. Hii ni baada ya Katango kurejea nyumbani akiwa amebeba uta na mata vitu ambavyo kulingana na utamaduni wao mwanamke hakupaswa kuvibeba. Katango naye anakabili suala hili kwa kusema kuwa vilikuwa ni mti tu kwa hivyo havingemsababishia madhara yoyote. Pia, katika mfano wa 36, Sakina anatumia mkakati ndani ya rekodi anapomwambia Ngwese kuwa alifanya kosa kwa kuwakataza Susa na Sota kuchota maji kisimani.

Katika sura ya pili, pia imebainika kuwa wahusika katika tamthilia hii teule walitumia mkakati wa utoupole wa matumizi ya kejeli. Kwa mfano, katika mfano wa 38, Katango anamwambia mamake kuwa baada ya Ngwese kuwakataza Susa na Sota kuteka maji, Ngwese ndiye aliyepaswa kuchaguliwa kuwa kiongozi. Hata hivyo mkakati huu wa matumizi ya Kejeli haujatumika sana katika tamthilia hii. Mwisho mkakati wa kutowasilisha chochote pia umetumika japo kama mkakati wa matumizi ya kejeli, haujatumika kwa wingi. Kwa mfano,

katika mfano wa 41, Kibwana anaamkuliwa na Kikubi lakini hajibu salamu. Anaendelea tu kusoma gazeti.

Madhumuni ya pili ya huu utafiti yalikuwa kubainisha namna mikakati ya utoupole inayotumiwa na wahusika katika tamthilia ya *Pango* inachangia katika ukuzaji wa sifa zao. Katika sura ya tatu madhumuni haya yamejadiliwa na kuafikiwa. Imebainika kuwa sifa za wahusika zinakuzwa wanapotumia mikakati mbalimbali ya utoupole. Kwa mfano, katika mfano wa 45, sifa ya Katango ya ujasiri inavyazwa kupitia mkakati hasi wa utoupole hasa anapoingilia faragha ya Ngwese na kumwambia kuwa babu yake alikuwa kibaraka wa wakoloni na aliwasaliti Waafrika kwa kushirikiana na wakoloni kuwahujumu Waafrika wenzake. Vilevile, katika mfano wa 46, kupitia mkakati hasi wa utoupole sifa ya Seki kama mhusika ambaye ni mhafidhina wa utamaduni inakuzwa. Hali hii inadhihirika baada ya Seki kumlaumu Katango kuwa alikuwa amekataa kupashwa tohara kwa mujibu wa desturi za jamii yake.

Aidha, kupitia mkakati chanya wa utoupole sifa za wahusika mbalimbali zimekuzwa kama inavyobainika katika sura ya tatu. Katika mfano wa 50, sifa ya Ngwese kama mhusika mwenye matusi inakuzwa anapomwuliza Katango kuwa alikuwa akibwekea nini pale. Matumizi ya lugha hii ya matusi yanakusudia kuvunja mawasiliano kati yake na Katango. Pia, Mfano wa 53, unakuza sifa ya Seki kama mhusika mbishi anapopinga kuwa Katango alisema uongo kuwa Ngwese aliwakataza wadogo zake kuteka maji kisimani.

Kupitia mkakati ndani ya rekidi wa utoupole unakuza sifa za wahusika mbalimbali ambao wanautumia katika maingiliano yao. Katika mfano wa 59, sifa ya Seki kama mhusika asiyejali hali ya mwanawe inabainika kwa kutumia mkakati huu wa ndani ya rekodi wa utoupole anaposema kuwa, anapotezewa wakati Katango alipokuwa akimweleza jinsi walivyoviziwa na watu waliodhaniwa kutumwa na Ngwese. Vilevile, kupitia mkakati huu wa kuwa ndani ya rekodi wa utoupole, sifa ya Ngwese kama mhusika mwenye ubinafsi inakuzwa kama inavyodhihirika katika mfano wa 61.

Mkakati wa matumizi ya kejeli pia umechangia katika kukuza sifa za wahusika. Kwa mfano, katika mfano wa 62, sifa ya Ngwese kama mhusika katili inakuzwa, Katango anapotumia mkakati huu akiongea na mamake kuwa ndiye kiongozi aliyefaa kuchaguliwa baada ya kuwakataza watoto wao kuteka maji kisimani. Hatimaye, mkakati wa kutowasilisha chochote wa

utoupole pia umetumika kuvyaza sifa za wahusika. Kwa mfano, kupitia mfano wa 64, sifa ya mama Katango kama mhusika karimu inakuzwa anapotembelewa na Kikubi na Kibwana na kwenda jikoni kuwaletea makopo ya uji na anaporejea anakuta washaondoka bila ya kumuaga.

Hatimaye madhumuni ya tatu ya utafiti huu ya kubainisha namna mikakati ya utoupole inayotumiwa na wahusika inaendeleza maudhui katika tamthilia ya *Pango* pia yameafikiwa. Kwanza, kupitia mkakati hasi wa utoupole anaotumia Seki katika mfano wa 65, unaendeleza maudhui ya utamaduni. Kwani Seki anatumia mkakati huu kuhasiri uso wa Katango anapomwambia kuwa aligomea kupashwa tohara. Kwa hivyo kwa mujibu wa utamaduni wa jamii yao ni kuwa wanawake walipashwa tohara na kitendo cha Katango cha kugomea utamaduni huu kiliwakera wahafidhina sana. Pia katika mfano wa 66, Katango anaendeleza maudhui ya usaliti, anapotumia mkakati hasi wa utoupole anapomwambia Ngwese kuwa babu yake alishirikiana na wakoloni kuwahujumu Waafrika. Kwa hivyo babu ya Ngwese aliwasaliti Waafrika wenzake.

Maudhui mbalimbali pia yamekuzwa kupitia mkakati chanya wa utoupole unaotumiwa na wahusika mbalimbali. Kwanza, katika mfano wa 70, Ngwese anatumia mkakati chanya wa utoupole kuhasiri uso wa Sakina hasa anapokataa ushirika wake kwa kumwambia kuwa arudi alikokuwa. Katika hali hii maudhui ya taasubi za kiume yanakuzwa. Kwani kulingana na Ngwese, kujibizana na mwanamke asubuhi ni kujiletea nuksi na siku nzima anaivuruga. Aidha, katika mfano wa 74, maudhui ya ubaguzi yanaendelezwa na Mtu 1 anapomwambia Katango akitumia mkakati chanya wa utoupole kuwa kigoda cha Pango mwanamke hawezi kukalia.

Mkakati wa ndani ya rekodi pia umetumika kuendeleza maudhui mbalimbali. Kwa mfano, katika mfano wa 76, maudhui ya utamaduni kandamizi yanaendelezwa. Hii ni baada ya Katango kuja nyumbani akiwa amebeba uta na mshale ambapo baba yake anamwambia kuwa wanawake hawakuruhusiwa kubeba vitu hivi kulingana na utamaduni wao. Mkakati huu pia umetumiwa kuvyaza maudhui ya ufiada kama inavyojitokeza katika mfano wa 79, ambapo Katango anawaonya wapiga kura dhidi ya kudanganywa na matunda waliotupiwa na Ngwese katika uwanja wa uchaguzi.

Mkakati wa matumizi ya kejeli nao umetumika kuendeleza maudhui ya ubinafsi kama inavyojitokeza katika mfano wa 80. Ambapo Katango anamwambia mama yake kuwa Ngwese

ndiye kiongozi aliyefaa kuchaguliwa baada ya kuwakataza Susa na Sota kuteka maji kisimani. Na mwisho, mkakati wa kutowasilisha chochote pia umechangia katika ukuzaji wa maudhui tofauti tofauti. Katika mfano wa 81, Kauleni anaendeleza maudhui ya usaliti kwani hata baada ya kusaidiwa kupata kiwanja alikojenga hoteli na Ngwese haonyeshi shukurani zozote. Kwani anashirikiana na mpinzani wa Ngwese kisiasa ambaye ni Katango. Kwa Ngwese huu ni usaliti.

Licha ya kwamba hii mikakati ya utoupole inayotumiwa na wahusika mbalimbali aliowaumba msanii inatusaidia kuelewa sifa zao na pia kuendeleza maudhui, inamsaidia msanii kujenga taharuki. Kwani kila mara mhusika anapotumia mkakati fulani wa utoupole, msomaji anakuwa na hamu ya kutaka kujua atakavyokabili mlengwa. Katika hali hii tamthilia hii haichoshi kuisoma.

5.3 Changamoto za Utafiti

Changamoto kuu iliyokabili utafiti huu ni ugumu wa uainishaji wa kauli za wahusika katika kategoria mbalimbali ya mikakati ya utoupole. Hali hii inatokana na ukweli kwamba kauli moja inaweza ikaanguka katika mkakati zaidi ya mmoja. Inabainika kuwa katika uchunguzi huu, kuna miktadha ambayo kauli ya mhusika inaweza ikaainishwa kama mkakati chanya wa utoupole na vilevile kama mkakati ndani ya rekodi wa utoupole. Hali kama hii inatokea ambapo kauli ya mhusika inajumuisha maneno yanayosetiri mikakati zaidi ya miwili ndani mwake. Tatizo hili mtafiti alilikabili kwa kuzingatia kauli hizi kama zenye kujumuisha mikakati mseto ya utoupole na hivyo kuichanganua kama kauli moja yenye mikakati mingi ya utoupole ndani mwake.

5.4 Mapendekezo

Mtafiti anapendekeza kwamba utafiti zaidi unaweza ukafanywa na watafiti wa baadaye kuhusu tanzu zingine za fasahi kama vile riwaya na hadithi fupi ili kubainisha namna mikakati ya utoupole inavyotumiwa na wahusika katika tanzu hizi. Pia, tunapendekeza kuwa utafiti mwingine ufanywe kukuhusu mikakati ya utoupole inavyotumiwa katika mitandao mbalimbali ya kijamii na washiriki wanapotoa maoni yao kuhusu masuala mbalimbali yanayojadiliwa humo. Aidha, mtafiti anapendekeza kuwa utafiti zaidi ufanywe kuhusu majukumu mengine ya mikakati ya utoupole katika kazi za fasihi.

MAREJELEO

- Brown, P. & Levinson, S. (1987). *Politeness: some universals in language usage*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Bousfield, D. (2008). *Impoliteness in Interaction*. Philadelphia: John Benjamin Publishing Company.
- Buliba, A. et al (2006). *Isimujamii kwa Wanafunzi wa Kiswahili*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Culpeper, J (1996). Towards an Anatomy of Impoliteness. *Journal of Pragmatics* 25 (3) : 349-367.
- Culpeper, J. (2001). *Language and Characterization: People in Plays and Other Texts*. London & New York. Routledge.
- Culpeper, J. (2005). Impoliteness and Entertainment in the Television Quiz Show : The weakest Link. *Journal of Politeness Research* 1:35-72.
- Culpeper, J (2011). *Impoliteness. Using Language to Cause Offence*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Culpeper, J., Derek, B. and Anne, W. (2003). Impoliteness Revisited with Special Reference to Dynamic and Prosodic Aspects. [http://id.scribd.com/doc/20554_1_12/Cupeper – impoliteness – revisited](http://id.scribd.com/doc/20554_1_12/Cupeper-impoliteness-revisited) .Retrieved on December 2 ,2016.
- Goffman, E. (1967). *Interaction Ritual*. Chicago: Aldine Publishing.

- Goro, M. (2014). *An Analysis of Impolite Language Used by Matatu Conductors: A Case Study of Matatus Plying Route 32 From Nairobi City Centre to Dandora*.Tasnifu ya Uzamili ambayo haijachapishwa: Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Grice, H.P. (1975). *Logic and conversation*. New York : New York Academic Press.
- Kinyua, G. (2015). *Ukiukaji wa Kanuni za Upole katika Mhanga Nafsi Yangu*.Tasnifu ya Uzamili ambayo haijachapishwa: Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Lakoff, R. (1973). The Logic of Politeness:Or Minding your P's and Q's.*Chicago Linguistic Society pp 292-305*.
- Lachenict, L. (1980). Aggravating Language: A Study of Abusive and Insulting Language. *International Journal of Human Communication 13:607-688*.
- Leech, G. (1983). *Principles of politeness*. London: Longman.
- Mey, J. (2009). *Concise Encyclopedia of Pragmatics*. Oxford: Elsevier Ltd.
- Mullary, L. (2008). Stop hassling me! Impoliteness, power and gender identity in the professional workplace. In D. Bousfield and M. Locher(eds.), *Impoliteness in Language: Studies on its Interplay with Power in Theory and Practice*, pp.1 , 16. Berlin and New York: Mouton de Gruyter.
- Muniu, G.G.(2013). *Ujagina wa Mwanamke Katika Pango*.Tasnifu ya Uzamili ambayo haijachapishwa:Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Nabelle, P. (2015). *A pragmatic Analysis of Impoliteness Strategies Used in Paranorman Movies*. Tasnifu ya Uzamili ambayo haijachapishwa: Chuo Kikuu cha Yogyakarta State.

Nyangi, L.C (2017). *Uchanganuzi wa Kipragmatiki wa Utoupole Katika Filamu za Kiswahili*.
Tasnifu ya Uzamili ambayo haijachapishwa: Chuo Kikuu cha Nairobi.

Nyangweso, M.S. (2017). *Nafasi na Athari za Kiongozi wa Kike Katika Tamthilia Teule za Kiswahili*.Tasnifu ya Uzamili ambayo haijachapishwa: Chuo Kikuu cha Maasai Mara.

TUKI (1990). *Kamusi ya isimu na lugha*, Dar-es-salaam: Educational publisher and Distributors.

Wafula, R. M. (1999). *Uhakiki wa Tamthilia: Historia na Maendeleo Yake*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Wafula, R. M. na Njogu, K. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Wamitila, K.W (2002). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers.

Wamitila, K.W (2003). *Pango*. Nairobi: Focus Publishers.